SportPesa
TZS. 595,659,980
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mitaa** yatengwa machinga Kariakoo kusubiri waendako

UKURASA 4




# Nipashe

Alhamisi Oktoba 21, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580740

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Mbappe: Rahisi sana kucheza na Messi**

UKURASA 23

# Sababu jaji wa pili kujitoa kesi Mbowe

• **Mapingamizi** yatupwa, Askofu awaombea mawakili, washtakiwa kabla ya uamuzi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### MADENI YA TTCL YAZIDI MALI ZAKE

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imebaini kuwa mapato ya baadhi ya kazi za Shirika la Mawasiliano nchini (TTCL) ikiwamo usambazaji wa mkongo...

UKURASA WA 5

### RC AZUIA MIL. 47/- ZIARA ZA MADIWANI

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameokoa Sh. milioni 47 ambazo zilikuwa zitumiwe na Baraza la Madiwani wa Jiji la Dodoma...

UKURASA WA 16

### KUNYONGWA HADI KUFA KWA KUUA MKE, KUMNYOFOA VIUNGO

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mbeya, imemhukumu kunyongwa hadi kufa Mateso Shantiwa, mkazi wa Kitusi wilayani Mbeya, baada ya...

## Mawasiliano ya Sabaya yafikishwa kortini

UKURASA 2



**Picha zote;** Askofu Emmaus Mwamakula wa Kanisa la Uamsho Moravian (kushoto), akiwafanyia maombi mawakili wa utetezi wa kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe na wenzake, kabla haijaanza kusikilizwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## PSSSF hoi, PAC yataka serikali kuilipa tril. 4.6/-

UKURASA 3

**MICHEZO** NABI ATETEA KUKATA PUMZI KIKOSI YANGA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake wakiwasili katika viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha jana, kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi namba 27, inayomkabili. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Mawasiliano ya Sabaya yafikishwa mahakamani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MENEJA wa Ulinzi wa Ushirika wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama Vodacom Tanzania Makao Makuu, James Wawenje (39), amedai mahakamani kwamba alipokea barua kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Arusha, ikiagiza kampuni hiyo kutoa taarifa za mawasiliano ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake wawili.

Meneja huyo ambaye ni shahidi wa sita wa Jamhuri, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi, mbali na Ole Sabaya, pia kuna washtakiwa wengine sita; Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41),Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29), Nathan Msuya (31), wanaokabiliwa na mashtaka matano.

Akiwasilisha ushahidi wake, Wawenje mwenye Shahada ya Udhamili ya Ulinzi aliyoipata Uingereza mwaka 2009, alidai kwamba barua hiyo ilitoka kwa Kaimu Kamanda wa TAKUKURU Mkoa wa Arusha, James Ruge, ikiagiza kampuni hiyo kuipatia taasisi hiyo mawasiliano ya Sabaya na wenzake wawili kutoka kwenye mfumo wa kupiga, kupokea simu na kutuma ujumbe mfupi kuanzia Januari 20 hadi Julai mwaka huu.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Othmed Mtenga, shahidi huyo alidai mahakamani kwamba Julai 20, mwaka huu, akiwa ofisi za kampuni hiyo, makao makuu walipokea barua kutoka kwa Kaimu Kamanda wa TAKUKURU, ikiomba taarifa za namba za siri za wateja waliokuwa wameorodhozeshwa.

"Baada ya kupokea niliingia katika mfumo wetu wa kupiga na kupokea kutoa ushirikiano kwa vyombo vya usalama kama ilivyokuwa desturi ya kushirikiana," alidai.

Shahidi huyo alionyeshwa nyaraka zenye taarifa za wateja wao hao na alizitambua na kuomba kupokewa kama kielelezo cha ushahidi mahakamani na mahakama iliridhia ombi lake.

Akisoma barua hiyo, iliamuru kutoa taarifa za mawasiliano ya kupiga na kupokea ujumbe mfupi za Lengai Ole Sabaya, Enock Togolani na Ramweli Macha kuanzia Januari 20 hadi Julai mwaka huu.

Shahidi huyo alidai mahakamani huko alipoingia kwenye mfumo wao, aliangalia namba hizo kama zipo katika mfumo wa usajili na alithibitisha kuwa ni namba za wahusika, hivyo alitoa taarifa kama barua kutoka TAKUKURU ilivyoelekeza.

"Baada kuthitibisha namba hizo kama zipo kwenye mfumo wetu wa usajili 'niliprint' taarifa hizo kwenye printa yetu ambayo ilikuwa salama na hakukuwa na hitilafu yoyote na mimi kama kiongozi wa kitengo cha ulinzi nilisaini taarifa hizo na kuandaa barua ya kuwajibu TAKUKURU na cheti ambacho kinaonyesha usalama wa mfumo na kugonga muhuri wa kampuni kuwakabidhi wahusika kama walivyoelekezwa," alidai.

Katika hatua nyingine shahidi huyo, alionyeshwa mahakama barua, taarifa za kupiga, kupokea na kutuma ujumbe mfupi na cheti cha kuonyesha usalama wa mfumo wakati wa kuchapisha taarifa hizo na aliomba mahakama kupokea kama vielelezo vya ushahidi mahakamani.

Baada ya ombi la shahidi huyo, mawakili wa washtakiwa wa kwanza na wa pili (Mosses Mahuna), wakili wa mshtakiwa wa tatu na wa nne (Fridolin Gwemelo) hawakuwa na pingamizi.

Wakili wa washtakiwa wa tano, sita na saba, Edmund Ngemela, alipinga kupokewa kwa baadhi ya vielelezo vya mfumo wa mawasiliano wa kielekroniki kati ya vile vilivyowasilishwa mahakamani kwa kuwa havikuambatana na cheti cha mifumo kuonyesha kama ilikuwa vizuri.

Shahidi huyo alisoma nyaraka zilizotolewa jana mahakamani zikionyesha mizunguko ya Sabaya ya Januari 22, mwaka huu.

Kwa mujibu wa nyaraka hizo, Saa 4:55 asubuhi Sabaya alidaiwa kuwa Bomango'mbe, Hai mkoani Kilimanjaro, akielekea Arusha.

Saa 6:53 mchana, alikuwa eneo la Kikatiti wilayani Arumeru mkoani Arusha, saa 6:54 alikuwa Ngayuku Hill Arusha, saa 7:11 mchana Usa River, saa 8:00 mchana Chuo cha Ufundi Arusha.

Siku hiyo hiyo, Sabaya alidaiwa kuwa saa 8:44 mchana, saa 8:59 mchana alikuwa Makao Mapya, saa 9:18 mchana alikuwa Matejoo na saa 9:24 mchana alikuwa JR Arusha.

# Sababu jaji wa pili kujitoa kesi Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imekataa mapingamizi mawili yaliyowasilishwa na mawakili katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, na wenzake watatu baada ya kubaini yanakosa mashiko.

Wakati uamuzi huo ukitolewa, Jaji Kiongozi Mustapha Siyani amejitoa kuendelea kusikiliza shauri hilo kwa sababu ya majukumu aliyonayo, akibainisha kuwa shauri hilo linatakiwa kusikilizwa mfululizo, hivyo kuwa ngumu kwake.

Jaji huyo amekuwa jaji wa pili kujitoa katika shauri hilo, Jaji wa kwanza, Jaji Elinaza Luvanda, alijitoa Septemba 6, mwaka huu, baada ya Mbowe kuomba afanye hivyo.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya Jaji Kiongozi Siyani baada ya kupitia ushahidi uliotolewa na mashahidi watatu wa upande wa mashtaka na mashahidi watatu wa upande wa utetezi pamoja na majumuisho yaliyowasilishwa na pande zote mbili.

Upande wa utetezi ulikuwa unapinga kupokewa kwa maelezo ya mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa, kwa madai yalichukuliwa nje ya muda na kwamba kabla na wakati yanachukuliwa mshtakiwa aliteswa.

"Mapingamizi yote mawili yanakosa mashiko kisheria, maelezo yalichukuliwa ndani ya muda wa saa nne, ushahidi wa utetezi unakinzana na pingamizi la pili, maelezo yalitolewa na mshtakiwa Adamu Kasekwa yalichukuliwa Kituo Kikuu cha Kati, Dar es Salaam kwa ridhaa yake," alisema Jaji Siyani.

Jaji Siyani alisema anakubaliana na matakwa ya kisheria kwamba maelezo yanatakiwa kuchukuliwa saa nne tangu mtuhumiwa awekwe chini ya ulinzi, yanapaswa kuanza kuhesabiwa.

Alisema kifungu cha Sheria Na. 51 Sura ya 20 na kifungu namba 50(2) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, muda umeongezwa na unaweza kuongezwa na mkuu wa upelelezi au kwa kuwasilisha maombi mahakamani.

"Kwa muktadha wa vifungu hivyo, lazima saa nne zizingatiwe labda tu kuwapo kwa maombi ya muda mahakamani, ukishindwa kuzingatia matakwa ya sheria namba 50 ushahidi huo haupaswi kupokewa.

"Katika shauri lililopo, Adamu Kasekwa alikamatwa Agosti 5, mwaka 2020 na maelezo yalichukuliwa Agosti 7 mwaka 2020, hakuna shaka saa nne zilipita, hakukuwa na ushahidi wa kuonyesha kwamba matakwa ya kisheria yalizingatiwa kwa kuomba muda wa kuongeza.

"Hakuna shaka kwamba mshtakiwa Kasekwa na Mohammed Ling'wenya walikuwa na Moses Lijenje maeneo ya Lau Madukani Moshi, mpango wa Kamishna Msaidizi wa Polisi Ramadhani Kingai na Inspekta Mahita Omary ni kuwakamata watu watatu lakini waliwakamata wawili na Kasekwa aliwaongoza kumtafuta Lijenje," alisema Jaji Siyani.

Alisema kwa maoni yake, dai la ACP Kingai kwamba baada ya kumkosa Lijenje walikuwa na juhudi za kumtafuta kujua alipo, ni vigumu kuondoa dhana kwamba Kasekwa alikuwa na askari kumtafuta Lijenje.

Jaji Siyani alisema hakuna ubishi kwamba Kasekwa alipokamatwa alisafirishwa Dar es Salaam na ushahidi wa Jamhuri unaunga mkono dhana ya kuwa muda uliotumika kumtafuta Lijenje Moshi na Arusha na muda uliotumika kumsafirisha haupaswi kuhesabika.

"Kwa maoni yangu, kifungu namba 51 kinapaswa kutumika pale unapoanza kumhoji, ikabainika muda hautoshi inawezekana kuomba kuongeza muda, hakuna ushahidi kwamba kulikuwa na mahojiano kabla ya Julai 7 mwaka 2020.

"Kifungu hicho hakipaswi kutumika sababu alikuwa hajaanza kuhojiwa. Kwa maoni yangu, kuchelewa kuhojiwa kulikuwa na sababu zinafanana na matakwa ya sheria.

"Hitimisho langu kwa pingamizi la kwanza, muda uliotumika kumtafuta Lijenje na kumsafirisha haupaswi kuhesabika kuwa sehemu ya saa nne," alisema.

Jaji Siyani alisema katika pingamizi la pili, jinsi lilivyowekwa mshtakiwa anakubali kutoa maelezo lakini si kwa ridhaa yake. Alisema ilikuwa wazi kwa upande wa utetezi kuomba maelezo yaliyotolewa Kituo cha Polisi cha Kati yapokewe.

"Maoni yangu ushahidi unakinzana na pingamizi, ushahidi wa Jamhuri unasema Kasekwa alifikishwa Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam na kuhojiwa na Kingai, Kingai aliomba kutoa maelezo ya Kasekwa aliyotoa kituoni hapo, pingamizi lingekuwa Kasekwa hakuwahi kutoa maelezo Kituo cha Kati.

"Kusema alitoa lakini kwa mateso maana yake alifikishwa na alitoa maelezo, ushahidi wa kwamba hakufikishwa alipelekwa Mbweni haupo mahakamani, maelezo yaliyoombwa kutolewa yalitolewa Kituo cha Kati," alisema.

Alisema mapingamizi yote mawili yamekosa mashiko kisheria, maelezo yalitolewa ndani ya muda wa saa nne, ushahidi wa utetezi unakinzana na pingamizi la pili.

Jaji Siyani alisema kitabu cha kumbukumbu hakikupingwa, ni dhahiri maelezo hayo yalitolewa na mshtakiwa Kasekwa kwa ridhaa yake, maelezo yaliyopingwa yalipokewa na kuwa kielelezo namba moja cha upande wa Jamhuri.

Baada ya uamuzi huo, alitoa mapumziko ya dakika 10 kujadiliana na mawakili kisha kurejea.

Aliporejea alisema baada ya uamuzi huo, shauri la msingi linapaswa kuendelea kusikilizwa na shahidi wa kwanza, ACP Kingai, ataendelea na ushahidi wake.

"Shauri hili ni moja ya mashauri yanayopaswa kusikilizwa mfululizo, kutokana na majukumu yangu ni vigumu kwenda mfululizo. Kwa sababu hii ili shauri liweze kuendelea kusikilizwa mfululizo, mimi najitoa atakuja jaji mwingine ataanzia nilipoishia.

"Shauri linaahirishwa mpaka Msajili atakapotoa tarehe ya kusikiliza na jaji atakayekuwa kapangiwa," alisema Jaji Siyani.

# PSSSF hoi, PAC yataka serikali ilipe tril. 4.6/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imesema hali ya Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) si nzuri na kutaka serikali kulipa madeni inayodaiwa ya zaidi ya Sh. trilioni 4.6 ili kuunusuru mfuko huo.

Vilevile, imeagiza kupatiwa ripoti ya tathmini ya uhimilivu wa mfuko huo ifikapo Novemba 30 mwaka huu ili itoe ushauri kwa serikali.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari mara baada ya mahojiano na watendaji wa mfuko huo kutokana na hoja za ukaguzi za mwaka 2019/20.

Alisema mfuko huo haupo vizuri kutokana na kudai madeni mbalimbali, hali inayosababisha kushindwa kujiendesha kwa ufanisi.

Kaboyoka alifafanua kuwa kuna deni la Sh. trilioni 4.6 ambalo serikali inadaiwa na mfuko huo zilizotokana na michango ya wafanyakazi walioajiriwa kabla ya mwaka 1999.

"Hawa wafanyakazi waliajiriwa na serikali kabla ya mwaka 1999 na walikuwa fedha zao hazipelekwi kwenye mfuko na serikali walisema watalipa fedha hizi lakini hadi leo hii fedha hizi hazijalipwa na kulifanya shirika lisifanye kazi zake vizuri," alisema.

Kiongozi huyo wa PAC alisema serikali pia ilikopa fedha kwenye mfuko huo kwa ajili ya kuwekeza kwenye ujenzi wa majengo mbalimbali ikiwamo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ambapo kuna fedha hazijarejeshwa kwenye mfuko huo kiasi cha Sh. bilioni 231 kati ya Sh. bilioni 731 zilizokuwa zinadaiwa.

"Matokeo yake ni kwamba shirika limeshindwa kufanya kazi kwa kiasi ambacho walikuwa wanataka wafanye kwa tija ya juu zaidi, tuna wasiwasi kwamba kama serikali haitaweza kulipa madeni hayo tutashindwa kujua kama shirika litaweza kufanya kazi au la," alisema.

Aliongeza: "Kamati mwaka jana iliagiza CAG afanye tathmini ya uhimilivu wa mfuko lakini ripoti haijatoka, ili kuangalia uhimilivu upo kiasi gani, na kama haujafanyika kamati tumeshindwa kujitosheleza kwamba shirika hili litaweza kufanya kazi kikamilifu."

Alisema PSSSF imewekeza fedha kwenye Benki ya Maendeleo (TIB) kiasi cha Sh. bilioni 86.1 na Dola za Marekani milioni 11.4 ambayo ni 'fixed deposit' na benki hiyo imeshindwa kuwalipa.

"Kwa maana hiyo ni kwamba TIB haitoi riba kwa sasa wala kurudisha fedha zao ambazo wameweka kwenye fixed deposit na hali ya TIB haijakaa vizuri, haieleweki kama watawalipa au sivyo,"alisema.

Aliagiza kufuatiliwa kwa madeni hayo na uwekezaji wa mfuko kwenye majengo hasa Twin Tower Dar es Salaam ambalo lina wapangaji wachache sana.

"Tumeliambia shirika hili wafanye juu chini na kuweka mikakati ya majengo hayo yaliyojengwa na fedha za mfuko kupata wapangaji ili fedha za kulipa mafao kwa wafanyakazi wakistaafu isilete utata, hatutaki mfanyakazi ifike muda wa kulipwa mafao yao hayapo,"alisema.

Alieleza kuwa mfuko kwa sasa unalipa zaidi kuliko unavyopokea mafao ya wafanyakazi.

"Ajira kwa muda mrefu hazipo wakati wastaafu wanaendelea kuwapo, kwa miaka mitano iliyopita ajira zilisitishwa, maana yake ni kwamba wale ambao wangekatwa fedha kwa ajili ya mfuko huu fedha hizo ndio ingelipa mafao ya wale wanaostaafu, imepungua sana, hilo nalo ni tatizo," alisema.

Alisema inahitajika mpango mkakati wa kuhakikisha mfuko huo unadumu ili usije ukashindwa kulipa mafao ya wastaafu.

## Madeni ya TTCL yazidi mali zake, PAC yagundua madudu ya mapato

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imebaini kuwa mapato ya baadhi ya kazi za Shirika la Mawasiliano nchini(TTCL) ikiwamo usambazaji wa mkongo wa taifa hazijaingizwa kwenye vitabu vya mahesabu, huku likiwa na madeni makubwa kushinda mali zilizopo.

Aidha, imetaka serikali kunusuru shirika hilo kwa kuliongezea mtaji au kuruhusu vyanzo vingine kwa TTCL ili kufanya kazi iliyokusudiwa.

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, aliyasema hayo jana mara baada ya kuhojiana na viongozi wa shirika hilo kufuatia hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za Mwaka 2019/20.

Alisema kuna viashiria vya moja kwa moja kwamba TTCL haifanyi vizuri hasa kutokana na hesabu zao zinavyoonekana.

"Imeonekana kuna baadhi ya kazi ambazo zinafanywa na TTCL na linalipa kodi na VAT lakini mapato yake hayajaingizwa kwenye vitabu vya shirika, kwa mfano mapato ya kusimamia Shirika la NIDC yaani Data Centre bado wanatumia namba ya mlipa kodi(TIN) ya TTCL na wafanyakazi wanatoka TTCL, mapato hayaingii kwenye vitabu, lakini inapokuja kwenye kulipa kodi TTCL wanalipa halafu baadae wanawadai wale hili halijakaa vizuri."

"Pia kuna kampuni NICT inasimamia mkongo wa taifa ambapo sisi kama kamati tuliamini unasimamiwa na TTCL sasa hizi kampuni mbili mapato yake yote hayajajumuishwa kwenye vitabu vya serikali," alisema.

**MAPATO KUTOINGIA VITABUNI**

Alisema kamati inaona kuna haja ya kukaa na serikali ili kufafanua kwanini mapato hayo hayaingii kwenye vitabu hivyo kwa mujibu wa sheria kwa kuwa TTCL ndio wasimamizi wa kazi hizo.

Aidha, alisema shirika lina mtaji hasi na lina madeni makubwa kushinda mali zilizopo.

"Tumefanya uchambuzi wa hesabu zao imeonekana kwamba mtaji wa kufanyia kazi unaonekana mtaji hasi wa Sh. bilioni 132, kwa hesabu za kitaalamu ukichukua mali za kawaida (current asset) kutoa current reliability unapata mtaji hasi madeni ni makubwa kushinda mtaji wa kufanyia kazi,"alisema.

Hasunga aliongeza: "Mtaji wao kwa ujumla ni Sh.Bilioni 242 wakati wa madeni ya Sh.Bilioni 403 kwa hiyo hicho ni kiashiria kwamba shirika haliendi vizuri."

Pia, Hasunga alibainisha kwamba soko halisi la TTCL halijakaa vizuri ikilinganishwa na washindani wengine.

## Kampuni za Ufaransa zakaribishwa nchini

**Na Mwandishi wetu**

TANZANIA imezihakikishia kampuni za Ufaransa kuwa mazingira ya biashara na uwekezaji ni salama na kuwasihi kuwekeza kwa wingi hapa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada baada ya kumalizika kikao kati ya Mawaziri wa Kisekta, wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Ufaransa na Tanzania, ikiwa ni ziara ya siku moja ya Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Kiutalii, Franck Reister,

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alisema serikali inajenga na inaendelea kuboresha mazingira rafiki ya uwekezaji kwa kuondoa kero mbalimbali zilizokuwa zinawakabili wawekezaji

"Tuna azma kubwa ya kuhakikisha tunajenga mazingira rafiki ya kuwekeza na kuondoa kero zote ambazo zimekuwa zinajitokeza ,kampuni nyingine zimeeleza kero hizo lakini tunafurahi zimeanza kuondolewa," alifafanua Balozi Mulamula.

Kwa mujibu wa Balozi Mulamula, Wafaransa wamekuwa na uhusiano mzuri na Tanzania kwa muda mrefu na sasa kuna shauku ya kufanya biashara na kuwekeza kwa wingi nchini.

Pia, alisema takwimu zinaonesha watalii kutoka Ufaransa kuja Tanzania kila mwezi ni zaidi ya 7,000 wanaokuja kutembelea vivutio mbalimbali, na kwamba ni wajibu wa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo.

Naye Waziri Riester alisema Ufaransa in kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji mambo ambayo pia yanatiliwa mkazo na Ufaransa.

"Ufaransa imedhamiria kuongeza ushirikiano na Tanzania na kama mlivyoshuhudia leo tumeanzisha safari za ndege za moja kwa moja kutoka Paris hadi Zanzibar ambazo zilisimama tangu mwaka 1974, huu ni mwanzo mzuri," alibainisha.

Kwa mujibu wa Riester, wataendelea kuwaeleza na kuwahamasisha wafanyabiashara na wawekezaji wa Ufaransa juu ya fursa mbalimbali zinazopatikana Tanzania ikiwamo katika sekta ya nishati, utalii, viwanda, usafirishaji na uwekezaji kuwekeza na kukuza uchumi wa pande zote mbili.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe:@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**DODOMA,**
**21/10/2021**

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatatu tarehe 25/10/2021** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam** kuelekea **Arusha,** gari yenye namba ya usajili: **KBV 558C/ ZD 9917**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **29.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.60** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port hadi Arusha Kupitia Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Manyara mpaka Arusha gari litasafiri muda wa mchana tu *(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*116522302*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe:@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**DODOMA,**
**21/10/2021**

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 22/10/2021** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari zenye namba za usajili: **T 210 BYM/ T 777 AQR/ T 836 DSC /T 837 CHK/ T 866 DDL /T 394 DVS/ T 996 DTN /T 393 DVS T 967 DTN /T 969 CPS/ T 680 DUB /T 390 DHQ/ T 296 CZS /T 974 CPS/ T 985 DTN /T 139 CHN/ T 684 DUB /T 387 DHQ**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **23.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.80** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port hadi Rufiji Kupitia Pwani, mpaka Rufiji gari zitasafiri muda wa mchana tu *(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*116522302*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Mitaa minne yatengwa machinga wa Kariakoo

**Na Maulid Mmbaga**

KUTOKANA na uhaba wa maeneo ya kufanyia biashara ndogo katika eneo la Kariakoo, uongozi wa wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, umetenga mitaa minne katika eneo hilo kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali hao.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Makamu Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Taifa, Stephen Lusinde, alisema mitaa iliyotengwa ni Kongo, Nyamwezi, Swahili na Sikukuu, na alibainisha kuwa maeneo hayo yatatumika kipindi cha neema cha siku 12 zilizotolewa na Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla, kwa machinga kuhamia kwenye maeneo yaliyo rasmi.

Alisema hadi sasa wamefanikiwa kwa zaidi ya asilimia 80 katika kutoa elimu juu ya suala la kuwapanga wafanyabiashara ndogo.

"Changamoto za hapa na pale zipo kwa sababu sisi ni binadamu, lakini ukizingatia mtu ana miezi sita au mwaka katika lile eneo kumhamishwa kidogo ni changamoto lakini tunaendelea kutoa elimu ili kuhakikisha kuwa zoezi hilo linafanikiwa," alisema Lusinde.

Pia alitolea ufafanuzi ugomvi uliojitokeza juzi katika eneo la Kariakoo wakati wakitimiza majukumu yao, akibainisha kuwa vurugu zilifanywa na vijana wahuni na sio wafanyabiashara.

Alisema vijana hao walikuwa na nia ovu ya kutaka kuharibu suala walilokuwa wakiliratibu.

"Kulikuwa kuna watu walitaka kutumika, sisi hatuwezi kutafsiri sana kuwa ni kisiasa au ni kwa namna gani kuhakikisha wanaharibu hili zoezi ambalo lina dhamira njema, walikuwa wanawarushia mawe viongozi wa machinga ili kutaka kuanzisha tafrani, hivyo ieleweke kuwa watu hao sio wamachinga halisi," alisema Lusinde.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Makalla, alisema utaratibu wa kuwapanga machinga katika mkoa huo umefanikiwa kwa kiasi kikubwa, akiwapongeza wafanyabiashara na viongozi wao katika baadhi ya maeneo kwa kukubali kuondoka na kushirikiana na serikali.

"Viongozi tumejifunza kwamba elimu ikitolewa, mkija na hoja haitohitaji nguvu na hiyo ndiyo siri ya mafanikio katika Mkoa wa Dar es Salaam.

"Wametuelewa, vibanda vingi vinavunjwa na wao wenyewe wanahama na kazi yetu sasa tumejipanga kuhakikisha kwamba kila eneo wanalohamia huduma za msingi kama umeme, maji, ulinzi na magari ya kushusha abiria katika maeneo hayo yanakuwapo ili biashara zifanyike.

"Leo (jana) mtu aliyekuja miaka mitano nyuma akaambiwa ile pale ndiyo IFM au CBE anaweza akahisi amepotea na kukuambia umempeleka sehemu nyingine, hata mji wenyewe ungekuwa ni binadamu tungesema umepumua kwa sasa.

"Ukiwa IFM una uwezo wa kuona Wizara ya Elimu lakini zamani kulikuwa vibanda, moshi kila sehemu kulikuwa na vurugu," alisema Makalla.



Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa barabara ya Makongo Juu, kwa kiwango cha lami, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CAG aagizwa ukaguzi maalum Momba

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imeagiza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba mkoani Songwe.

Ukaguzi huo unatokana na kubainika kuwapo na kiwango kikubwa cha udanganyifu wa zaidi ya Sh. milioni 500, shida kwenye ununuzi na ukiukwaji wa usimamizi katika Soko la Kimataifa la Kakosi.

Kamati hiyo pia imebaini vitendo vya makusudi vya kukosea kujaza fomu za madai za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na kuandika taarifa za uongo jambo ambalo linasababisha kutolipwa fedha.

Akizungumza jana kwenye kikao cha kamati hiyo, Makamu Mwenyekiti wa LAAC, Selemani Zedi, alisema taarifa ya CAG imebaini dosari kadhaa kwenye eneo la ununuzi ikiwamo ununuzi kufanyika kwa fedha taslimu bila idhini ya bodi na ushindani.

"Maagizo ya kamati ni kwamba Ofisi ya CAG iende Momba, maana mmetoa maelezo kwamba ofisa ununuzi aliyekuwapo hakuwa na vigezo na kwa sasa mmepata ofisa mwingine lakini tunajua kwamba ununuzi ni mchakato unaohusisha watu wengi.

"Kwa hiyo mkaguzi aende Momba akafanye ukaguzi maalum kwenye eneo hili ili kubaini hasa shida ilikuwa ni nini?," alisema. Kuhusu soko la Kakosi, Zedi alisema limetumia fedha Sh. bilioni nane na taarifa ya ukaguzi imebaini ukiukwaji kwenye usimamizi.

"Pia maelekezo kwa CAG akaingie kwa kina kukagua ili tujue nini kilitokea pale. Lakini kuna fedha za EP4R ambazo mwaka mzima zimekaa hazijatumika na maelezo yenu mnasema hamjazipokea hizo fedha lakini taarifa ya CAG ya mwaka 2020/21 amekuta salio anzia(opening balance) sasa kama hamjapokea hela hiyo opening balance imetoka wapi.

"Kuletewa fedha zinazopaswa kujenga madarasa lakini zinakaa mwaka mzima jambo ambalo halipo sawa, NHIF maelekezo ya kamati fedha hizi zilipwe lakini tunaona Halmashauri haichukui hatua zozote, kwa kuwa wanaokosea ni watumishi wa Halmashauri sasa tunaagiza wabainishwe na fedha zilipwe," alisema.

Alisema upelekaji wa asilimia 40 ya makusanyo kwenye miradi ya maendeleo, taarifa ya CAG imebaini Halmashauri ya Momba kwa mwaka wa fedha 2019/20, haikupeleka ipasavyo kiwango hicho.

"Taarifa imebaini kwamba imepeleka asilimia tano tu ya kilichopaswa kupelekwa, hamkupeleka Sh. milioni 455 ambayo mlikuwa mnatakiwa kupeleka na mmekiri. Hili ni kosa na mmesema kuanzia sasa kwenda mbele mtakuwa mnatenga hii fedha kwa kila mnachokusanya kwa mwezi ili mwisho wa mwaka ukifika hii asilimia 40 iwe imepatikana," alisema. Alisema kamati hiyo haitapokea utetezi wowote kuhusu Halmashauri kutopeleka asilimia 40 kwenye miradi hiyo kwa kuwa ni mwongozo wa TAMISEMI unatakiwa kutekelezwa.

Kuhusu sheria ya kutenga asilimia 10 ya makusanyo kwa ajili ya vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu, alisema taarifa za ukaguzi zinaonesha kwa miaka miwili bado Momba hawapeleki kikamilifu.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Grace Tendega, aliitaka halmashauri hiyo kutekeleza ipasavyo maelekezo hayo ya kamati, kujitathmini na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi.

## 'Wahitimu vyuo msisubiri ajira'

**Na Gwamaka Alipipi**

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) amewataka wahitimu wa vyuo vikuu nchini kutosubiri kuajiriwa na serikali bali wawe wepesi kuangalia ni wapi ujuzi wao utatumika kwa ufanisi zaidi, hata ikiwezekana wafanye kazi za kujitolea.

Prof. Willium Anangisye alitoa rai hiyo jana wakati wa mahafali ya 51 ya chuo kikuu hicho.

Alisema kwa kufanya hivyo wahitimu wa vyuo vikuu watajenga kujiamini, ujuzi na mchango wao utatambuliwa na kuinufaisha jamii.

"Tumieni elimu yenu kama ushawishi kwa watu wote ili muwe chachu ya mabadiliko katika jamii yetu. Kumbukeni kuwa elimu na maarifa mliyoyapata ni mali ya umma. Elimu na maarifa haiwezi kuwa chachu ya mabadiliko yaliyokusudiwa kama haitatumika katika kutatua matatizo ya jamii," alisema Prof. Anangisye.

Vilevile, aliwataka wahitimu wa vyuo vikuu pindi wanapojiunga na jamii kama sehemu ya nguvukazi, wawe wepesi wa kujifunza mambo mapya na kubadilika kwa haraka, ili wasiachwe na wakati.

Prof. Anangisye alisema: "Jitahidini kudumisha sifa ya UDSM popote mtakapokuwa, kwa kuwa chachu ya maendeleo na mifano ya kuigwa na wengine. Kamwe msishushe hadhi ya chuo kwa kufanya jambo lolote lisilofanana na sifa na umaarufu wake."

Vilevile, aliwataka wahitimu hao kuwa watu wa kutafuta fursa badala ya kusubiri fursa kuwafuata, akisema kuwa jambo hilo siyo rahisi kutokea katika ulimwengu wa leo.

Pia aliwataka wahitimu hao kuwa na hulka ya kudhubutu kujaribu mambo ambayo yanaonekana ni magumu, kwamba hata pale watakaposhindwa kufikia mafanikio yao wasife moyo.

"Mnapokwenda mtaani muendelee kuchukua tahadhari zote za virusi vya corona sambamba na kuchanja chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo kwani bado upo na unaleta madhara katika jamii," alisema Prof. Anangisye.

Mwenyekiti wa Baraza la UDSM, Jaji Mstaafu Damian Lubuva, aliwataka wahitimu hao kwenda kutumia ujuzi walioupata, kujifunza na kushirikiana na jamii.

Jaji Lubuva alisema: "Mazingira ya sasa ni tofauti na miaka ya nyuma, wakati sisi tunasoma tulikuwa tumeshaandaliwa ajira, lakini kwa miaka ya sasa ni lazima utafute ajira, lakini msisubiri kuajiriwa, tumieni ujuzi wenu kujiajiri."

Jaji Lubuva pia aliwataka wahitimu hao kwenda kuwa mabalozi wazuri wa UDSM katika jamii sambamba na kuendelea kuchukua tahadhari ya magonjwa ya milipuko.

Hivi sasa kunashuhudiwa tatizo la uhaba wa ajira miongoni mwa wahitimu wa elimu ambalo kuhalisia linazikumba nchi nyingi duniani.

## HABARI KITAIFA

# Mtaka azuia matumizi milioni 47/- za ziara ya mafunzo madiwani

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameokoa Sh. milioni 47 ambazo zilikuwa zitumiwe na Baraza la Madiwani wa Jiji la Dodoma kwenye ziara za mafunzo katika mikoa ya Mbeya na Arusha.

Sambamba na kuokoa fedha hizo, Mtaka amekemea lugha chafu zinazotolewa na baadhi ya wafanyakazi wa jiji kwa wateja wanaofika kupata huduma katika ofisi za umma.

Mtaka aliyasema hayo jana katika kikao kazi cha watumishi wa Jiji la Dodoma kilichofanyika kwa lengo la kutatua matatizo yaliyopo katika ofisi hiyo pamoja na kujadili hali ya utendaji kazi.

Alisema amezuia matumizi ya Sh. milioni 47 ambazo zilikuwa zitumiwe na madiwani kwa ajili ya mafunzo kwenye mikoa hiyo.

"Hivi katika kipindi hiki wapo watu ambao hawajui serikali inahitaji nini kwa ajili ya maendeleo? Rais anakemea matumizi mabaya ya fedha katika hotuba zake, lakini nawashanga ninyi wenzetu wa jiji hili," alisema.

Mkuu wa mkoa alibainisha kuwa alipata barua ya baraza hilo kuhusu kuomba kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kufanya ziara ya mafunzo Mbeya, Kilimanjaro na Arusha.

Pia alisema barua hiyo ilieleza kuwa lengo la mafunzo hayo ilikuwa kujifunza namna ya ukusanyaji wa mapato na uendeshaji wa shule za michepuo wa Kiingereza.

Alisema mambo mengine yaliyoelezwa kwenye barua hiyo ni pamoja na kujifunza namna ya kuondoa daraja sifuri katika matokeo ya mitihani mbalimbali na usafi wa mazingira.

Fedha hizo, aliongeza kuwa zilikuwa zitumike kwa madiwani 55 pamoja watumishi 14, hivyo gharama hizo zingetumika kama posho na mafuta ya magari kwa safari ya watu 69.

Katika kikao kazi hicho, Mtaka alikemea lugha chafu na kejeli zinazotolewa na baadhi ya wafanyakazi wa jiji hilo kwa wateja wanaofika kupata huduma.

"Ofisi ya Jiji imejaa lugha za kejeli na za ovyo kuanzia kwa wateja na wenyewe kwa wenyewe ninawaonya acheni tabia hizo," alisema.

"Ikijitokeza waziri au kiongozi mwingine akajibadilisha na kuingia ofisi ya Jiji la Dodoma, atawafukuza wengi kutokana na tabia zenu hizo za lugha chafu na za ovyo ndiyo maana tumeitana hapa kabla ya kuanza kuchukuliana hatua za kinidhanmu na kisheria," alisisitiza.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema ameitisha kikao kazi hicho kwa lengo la kukaa na wafanykazi wote wa kila idara kuwaeleza baadhi ya kero zilizopo pamoja kusikiliza kero za watumishi hao.

Aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanatatua kero za wananchi na kusimamia miradi ya maendeleo iliyokusudiwa.

Mkurungenzi wa Jiji, Joseph Mafuru, alisema kuna wafanyakazi 4,300 na waliohudhuria kikao kazi hicho ni wafanyakazi 1,500 kutoka idara za utumishi, mipango miji, ardhi, mazingira, TEHAMA, maendeleo ya jamii, uchumi, nyuki, kilimo, mifugo, uvuvi na ukaguzi.

# Ufaransa yahakikishiwa ushirikiano wa kibiashara

**Na Salome Kitomari**

TANZANIA imeihakikishia Ufaransa ushirikiano na kuimarisha kubadilishana uzoefu na teknolojia katika nyanja zote zenye manufaa kwa wananchi wa pande zote.

Mbele ya Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Kiuchumi wa Ufaransa, Franck Reister, juzi mawaziri watatu: Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, Waziri wa Uwekezaji na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Balozi Liberata Mulamula, walihakikishia Ufaransa ushirikiano huo.

Waziri huyo aliambatana na ugeni kutoka nchini humo akiwamo Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, ambao walizindua maduka yanayomilikiwa na kampuni ya Kifaransa ya Lagadere Travel Retails iliyoshirikiana na ya nchini Bevco Limited katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, Terminal Three.

"Naomba kuwahakikishia wafanyabiashara wote wanaofanyakazi kwenye viwanja vya ndege vyetu tuna-tendelea kuwapa heshima, fursa na kushirikiano ili tuendelee kupata wateja wengi na serikali tupate faida kubwa," alisema.

Waziri Mkumbo alimshukuru waziri huyo na kubainisha kuwa kampuni zinazowekeza nchini ni mabalozi kwa wawekezaji wengine duniani kuwekeza nchini.

Akizungumza baada ya kuzindua duka hilo, Waziri Reister alisema maduka hayo ni alama ya ukuaji wa biashara kwenye uwanja huo na kwamba ni mfano mzuri wa ushirikiano baina ya nchi hizo.


# NOTISI / TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | NEEMA ELINIMO MSWIA | TOYOTA RAUM T294 CWU | NEEMA ELINIMO MSWIA | KIMARA | 10/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | DICKSON ANICETH GREEN | NYUMBA | DICKSON ANICETH GREEN | ILEMELA MWANZA | 05/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA (2)<br>2.KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA, BUGARIKA IGELEGELE WILAYA YA NYAMAGANA MWANZA<br>2.NYUMBA ,BUGARIKA MWANZA<br>3.KIWANJA , BUJINGWA MANISPA YA ILEMELA | 1.12/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA<br>2.12/11/2021 SAA 10:00 JIONI NA KUENDELEA<br>3.13/11/2021 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| MWANZA | JEFTA NYASA MALULU | NYUMBA (2) NA BOMA | JEFTA NYASA MALULU | ZIPO KATIKA KIWANJA NAMBA 2685 KITALU ''A" EAST NYASAKA MANISPAA YA ILEMELA, MWANZA | 09/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | EDWARD NYAKANYA MSOGOLO | KIWANJA | ROSE ELIAS KISUMO | KIWANJA NAMBA 121 KITALU "5" BUGARIKA JIJI LA MWANZA | 10/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MICHAEL OCHIENG OTANG | NYUMBA | MICHAEL OCHIENG OTANG | HATI YA MAUZIANO – NUNDU MECCO ILEMELA MWANZA | 16/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | NYERERE JACKSON MWERA | 1.GARI ISUZU JOURNEY T354 DRT 2.GARI NISSAN CIVILIAN T357 DRT | NYERERE JACKSON MWERA | MWANZA | 05/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ROBERT THOMAS SERERYA | 1.KIWANJA 2.NYUMBA 3.KIWANJA CHENYE MSINGI | ADELA PETER EZEKIEL | 1. KISHILI NYAMAGANA MWANZA 2.KANGAYE ''A" NYAKATO ILEMELA MWANZA 3. NSUMBA ILEMELA MWANZA | 1.15/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA 2.15/11/2021 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA 3.15/11/2021 SAA 10:00 JIONI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MARIANA PATRICK SEDA | NYUMBA | MAILA MICHAEL BINA | KINYAMWEZI PUGU | 11/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | AMA ABDALLAH KIPENDE | NYUMBA | AMA ABDALLAH KIPENDE | KISARAWE | 12/11/2021 SAA TANO ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MATHIAS MHANGINONYO | NYUMBA | MATHIAS MHANGINONYO | KITUNDA | 24/11/2021 SAA TANO ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ZUBERI OMARY KIROBOTO | NYUMBA | MEDADUS LEON SHAO | MTONI MTAA WA BUSTANI | 23/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JAMILA KONDO GEMA | NYUMBA | JAMILA KONDO GEMA | KIPUNGUNI | 25/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | NEEMA LUCAS NDIFA | NYUMBA | NEEMA LUCAS NDIFA | NGWALE -CHANIKA | 26/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | BOSCO STEPHEN MHAGAMA | NYUMBA | BOSCO STEPHEN MHAGAMA | KIFURU | 27/11/2021 SAA TANO ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | HALPHAN JAFARI JUMA | NYUMBA | HALPHAN JAFARI JUMA | MIEMBE SABA 'B' KIBAHA | 29/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SHABANI JUMA MAGAZI | NYUMBA | SHABANI JUMA MAGAZI | KILIMAHEWA -KIBAHA | 15/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | OMARI SAIDI MNEMBWE | NYUMBA | OMARI SAIDI MNEMBWE | MAILI MOJA KIBAHA | 23/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | DOTO HARUN MSUYA | NYUMBA | DOTO HARUN MSUYA | TANGINI KIBAHA | 17/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ERNESTER FESTO MASAE | NYUMBA | DOROTHEA BEATUS GABRIEL | VIKONGORO-CHANIKA | 18/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | HONESTY LUDOVICK FRANCE | NYUMBA | HONESTY LUDOVICK FRANCE | TEGETA 'A' | 19/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | KIBA AMON MANIAMBA | NYUMBA | KIBA AMON MANIAMBA | MWAKITETE-MBEYA | 10/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0743885084/ 0714939933/ 0718038313
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

21652502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabilioni ya TASAF yaonyeshe uhalisia maisha ya wanufaika

**HIVI** karibuni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), uliieleza umma kuwa umepokea Sh. bilioni 5.5 kama fedha za masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kutekeleza mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Wanufaika wa fedha hizo ni kaya 40,740 waliopo kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini kwenye miji na majiji, ambao walipata athari ya UVIKO-19 katika shughuli zao.

Mradi wa kunusuru kaya maskini ni katika halmashauri 184 Tanzania Bara, Unguja na Pemba zenye kaya milioni 1.4 zenye watu milioni 10 wanaotoka kwenye mazingira magumu, wanaopatiwa ruzuku ya kujikimu, kufanya kazi kwenye miradi ya jamii na kulipwa ujira ambao unaziongezea kipato na kuunganishwa kwenye vikundi vya kujiwekea akiba.

TASAF imesema imejipanga kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa walengwa wa mpango unaanza haraka, na kutakuwa na ufuatiliaji wa karibu. Tunapongeza uamuzi wa kusaidia wananchi maskini ili kuwatoa kwenye umaskini na kupunguza idadi ya watu wanaoishi kwenye hali ngumu, ambao watamudu mahitaji ya familia zao na kuchangia uchumi wa nchi.

Tunatarajia fedha hizi zitatumika ipasavyo ili tathmini itakapofanyika ionyeshe namna gani mradi hiyo ilibadili maisha ya walengwa kama ilivyokuwa TASAF I na II, ambazo zilijenga vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, zahanati, vituo vya afya na miundombinu ya barabara kulingana na kipaumbele cha wakazi wa eneo husika.

Kwenye miradi hiyo wananchi walichangia nguvu kazi ya asilimia 20 na TASAF ilitoa asilimia 80 ya fedha za mradi, na hadi sasa ipo kwenye vijiji mbalimbali na manufaa yake yanaonekana.

Ni muhimu fedha nyingi iwafikie walengwa na miradi ionekana na siyo kutumika kwenye shughuli za uendeshaji ambazo nyingi ni kulipa mishahara, posho na gharama nyingine kama za malazi na nauli.

Tunatambua kuna watu wanaowajibika wanapaswa kulipwa, lakini ni vyema itakapofanyika tathmini basi wanufaika waonekane kunufaika na mradi hiyo, na iwe imewavusha katika hali za maisha kutoka hali walizokuwa nazo awali. Ni muhimu Sh. bilioni 5.5 zikaonekana kwenye maisha ya watu na mabadiliko yaonekane kuliko familia hizo kuendelea kubaki katika hali ngumu.

Moja ya miradi wanayofanya wanufaika wengi ni ufugaji wa kuku, sawa ni mradi mzuri, lakini ni lini ufugaji wa kuku wawili au watatu utamchomoa mtu kwenye umaskini, akaweza kutimiza mahitaji ya familia yake?


Wengine wanaanzisha kuuza bidhaa mbalimbali ambazo kimsingi bado hazileti matokeo makubwa kwenye maisha yao, kwa kuwa wanatakiwa kutunza familia zao kwa mahitaji ya msingi kama kusomesha watoto na kulipia huduma nyingine.

Tunatarajia kuona wanufaika wanajivunia kiuhalisia mabadiliko ya maisha yao, kwamba mtu alikuwa hawezi kusomesha wanawe sasa analipa ada au anaweza kujilipia gharama za matibabu.

Ikiwa fedha nyingi kati ya hizo zitatumika kugharamia shughuli za uendeshaji, maana yake fedha kiduchi ndizo zitakwenda kwa walengwa, ambao wanapaswa kuonyesha mabadiliko na kuondoka kwenye mstari wa umaskini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Elimu chanjo iende sambamba na namna ya kupata lishe bora

Na Mary Geofrey

**KUANZIA** Oktoba 18 hadi 23 mwaka huu, ni Wiki ya Lishe Kitaifa, ambayo maadhimisho yako yanafanyikia mkoani Tabora.

Taasisi ya Chakula na Lishe, inaadhimisha wiki hii kwa kuhimiza watu kuzingatia mlo kamili ulio katika makundi matano muhimu ya chakula.

Hapo kuna vyakula; vyakula vya asili ya nafaka, mizizi, ndizi mbichi, kundi la pili ni vyakula vya asili ya wanyama na jamii ya kunde; tatu ni mboga; nne matunda; na la tano ni sukari, mafuta na asali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Dk. Germana Leyna, anasema wiki hiyo ina lengo la kuhimiza wananchi kwa mlo kamili, ili kuepuka kushambuliwa na maradhi mbalimbali.

Anasema, maambukizi ya UVIKO-19 yameakisi hali ya lishe kwa Watanzania siyo nzuri, kutokana na namna yanayowaathiri wengi, hata baadhi kupoteza maisha.

Mkurugenzi anasema, lishe bora inasaidia kuimarisha kinga ya mwili na kupunguza ukali wa maradhi pamoja na vifo vitokanavyo na magonjwa ya kuambukiza ikiwamo UVIKO-19.

Anatumia fursa hiyo kuwataka wananchi wazingatie mlo kamili kutoka katika makundi tajwa, ili waepuke maradhi mbalimbali yasiyo ya kuambukiza na kuambukiza ikiwamo Utapiamlo na Kiribatumbo.

"Hivyo Siku ya Lishe Kitaifa ni jukwaa muhimu katika kutekeleza na kuendeleza azma ya serikali kutokomeza aina zote za utapiamlo nchini na kuendeleza jitihada za serikali," anasema Dk. Leyna.

Mtaalamu huyo wa lishe anasema pia maonyesho hayo yatachangia kuongeza uelewa na ufahamu kuhusu lishe bora na hatua chanya hususani katika ngazi ya kaya na jamii.

Anasisitiza kuwa, pia wanaendelea kutoa dawa za kutibu wagonjwa wenye utapiamlo mkali na kadiri, kuanzisha siku maalum ya kuadhimisha mafanikio ya jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na kuendelea kuhamasisha umma kwa kutoa elimu kuhusu faida za lishe bora na athari zake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Aidha, maadhimisho hayo ambayo kilele chake ni Oktoba 23 yana kauli mbiu inayosema 'Lishe Bora ni Kinga Thabiti dhidi ya Magonjwa; Kula Mlo Kamili, Fanya Mazoezi, Kazi Iendeleee'.

Anasema, katika kutilia mkazi umuhimu wa elimu kwa jamii, watatoa mafunzo kwa vitendo namna ya kuandaa na kupika vyakula vinavyozingatia mlo kamili ambayo inajenga afya ya mwili.

Ofisa Lishe Mtafiti Mwandamizi wa TFNC, Hamida Mbilikila, anasema mwili na kingamwili vikiwa imara vinasaidia kuzuia athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza na maambukizi ya Covid-19.

Mbilikila anaendelea kusema kuwa, virutubisho aina ya protini husaidia mwili kutengeneza chembe chembe au seli mpya na kukarabati seli za mwili zilizoharibika, kuimarisha mfumo wa kingamwili.

Ili kupata protini, vitamini na madini kwa wingi, mtu anapaswa kula kwa wingi vyakula vya asili ya wanyama, mboga na matunda.

Wote tunafahamu kuwa kazi inayoendelea ni kupata chanjo ya kujikinga na UVIKO-19 ambako Oktoba 8 mwaka huu serikali ilipokea dozi 1,065,600 ya chanjo aina ya Simnopharm kutoka nchini China.

Kazi kubwa inayoendelea ni kuhimiza watu kufahamu umuhimu wa chanjo ili wachanje na kuepuka ili wasispate kuambukizizwa makali yanayoweza kusababisha watu kuendelea kupoteza maisha.

Wadau wa afya na serikali wameungana na Rais Samia Suluhu Hassan kuwatoa hofu wananchi ili wachanje jambo litakalosaidia kupunguza maambukizi.

Juhudi zinazofanyika ni kubwa na tunasikia na kuona kupitia vyombo mbalimbali vya habari lakini ni vizuri sasa juhudi hizi zikaenda sambamba na kuhimiza jamii kula mlo kamili.

# DC ataja chanzo uharibifu misitu

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, amesema chanzo cha uharibifu wa misitu ni shughuli za kibinadamu na kwamba dawa ya kumaliza tatizo hilo ni kuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi.

Ngoma alisema hayo juzi alipokuwa anafunga kikao kazi cha kuwajengea uelewa viongozi na wataalam wa misitu wa Wilaya za Nachingwea, Ruangwa na Liwale, ambazo programu ya mnyororo wa thamani wa misitu (FORVAC) inafanya nazo kazi. Kikao hicho kilifanyika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi.

Alisema ili misitu iendelee kuwapo, kuna umuhimu kwa wananchi wakawekewa utaratibu ikiwamo mpango mahususi wa matumizi bora ya aridhi.

Akifunga kikao hicho kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zaynab Telak, alisema kuwapo kwa mpango huo kutasaidia pia watu kuwaweka katika utaratibu mzuri na unaohitajika, hivyo kupunguza tatizo la kutoweka kwa misitu kunakochangiwa na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji na uvunaji wa mazao ya misitu bila utaratibu.

Ili binaadamu na viumbe vingine viishi, alisema misitu inahitajika kuwapo kwa kuwa kuna faida kubwa ikiwa ni pamoja na kuzuia mmomonyo wa ardhi, kuchangia vivuli, kuleta maji ya mvua, huku akiipongeza FORVAC kwa jitihada za kusaidia utoaji elimu ya utunzaji wa misitu kwa wananchi.

Mkuu huyo wa wilaya alisema ongezeko la idadi ya watu na mahitaji yao ni miongoni mwa sababu zinazochangia utowekaji wa rasilimali misitu katika maeneo mbalimbali ya Wilaya, Mkoa na maeneo mengine.

"Kutokana na ongezeko hilo, kuna uhitaji mwingi unayohitajika, kama vile kilimo, ufugaji na kuna watu wanapoiona miti basi upandwa na Shetani na kutaka kuikata," alisema Ngoma.

# Mawakala forodha wataja sababu kukosa biashara kwa miaka miwili

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Mawakala wa Forodha Tanzania (TAFFA) kimesema biashara kwa wanachama wake imekuwa ngumu kutokana na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kufanya kazi zao.

Rais wa TAFF, Edward Urio, aliwasilisha kilio chao hicho jana jijini Dar es Salaam katika mkutano mkuu wa chama hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari, Urio alisema Sheria ya TASAC ya Mwaka 2017, imechukua asilimia 45 ya kazi ambazo wanazifanya.

"Kupitia mkutano huu, tutawaeleza wanachama wetu kwamba tupo katika mchakato na serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kuangalia ni namna gani sheria hii itaboreshwa ili iwe na tija kwenye uchumi wa taifa.

"TASAC imetuathiri kwa sababu kama nilivyosema asilimia 45 ya majukumu yetu wameyachukua, bado kuna mwingiliano wa kimaslahi, kwa bahati mbaya yeye ni mshindani wetu na pia ni mdhibiti," alisema.

Kiongozi huyo alisema siyo zaidi ya bidhaa tano ambazo zina maslahi na serikali lakini sasa zimechukuliwa na TASAC.

"Mfano, wanyama hai ililenga kama simba, twiga, mamba, nyoka lakini kwa sababu sheria haijafafanua, TASAC imechukua wanyama wote wanaoingia nchini ikiwamo vifaranga vya kuku, mbuzi na ng'ombe tunaopeleka Comoro," alifafanua.

Alisema kwa sasa wapo kwenye majadiliano na serikali chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi na tayari wameshafanya vikao takribani vitatu.

"Serikali imekusanya maoni yetu kuhusu sheria hii na ni mategemeo yetu wakikamilisha mchakato wa kuiboresha sheria wataita wadau ili wapitishwe kwenye mabadiliko ya muswada kabla ya kufuata hatua nyingine," alisema.

Rais huyo alisema wamemwandikia barua Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), kuangalia upya kama wanachama wao wanaweza kupewa leseni za miaka mitatu badala ya mmoja zinazotolewa hivi sasa ili wakopesheke kwenye taasisi za fedha.

"Kama mnavyojua miradi mikubwa ya serikali iko njiani kuja na asilimia 60 ya bajeti ya miradi hii ipo kwenye mambo ya kiforodha na usafirishaji, tunategemea fursa kubwa kama hizi wanachama wetu wazifaidi, watazifaidi vipi kama hawana mitaji au wana leseni za mwaka mmoja?" Alihoji.

Kuhusu corona, alisema iliporipotiwa kwa mara ya kwanza mwaka jana, waliathirika kwa sababu dunia nzima walifunga lakini kwa sasa milango imeanza kufunguka.

Rais wa Jumuiya ya Wakala wa Forodha Zanzibar, Omari Hussein Musa, alisema kwao matatizo yaliyopo ni suala la corona lakini kwa sasa nchi nyingi zimeanza kufunguka.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Sprint Cargo, Robert Mushi, alisema kitendo cha TASAC kufanya biashara wanazozifanya wao, kinawafanya wakose imani kwa sababu wanashindwa kuwashirikisha kila kitu kwa kuwa tayari ni mshindani wao.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Ikumo Clearing and Logistics, Ikupa Njela, alisema matatizo makubwa wanayokumbana nayo ni namna ya upataji kazi kwa sababu nyingi zimerudi mikononi mwa TASAC.

"Ushauri wetu tunawaomba TASAC wasimame kama taasisi inayosimamia mawakala wa forodha, wasifanye kazi, wachague moja, kutusimamia au kuwa washindani wetu wa kibiashara. Hali ya biashara karibu miaka miwili siyo nzuri, na corona ilivyoanza wafanyabiashara hawasafiri kuleta bidhaa," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (kulia), akikabidhi zawadi ya Sh. milioni 10 kwa Salma Said aliyeibuka mshindi wa bahati nasibu ya Biko maarufu kama buku nibukue, katika Benki ya NBC Tawi la Victoria, mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja Masoko wa Biko, Goodhope Heaven (kushoto) na Balozi wa Biko, Kajala Masanja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri zasisitizwa mipango urithishanaji madaraka

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAIMU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Hassan Kitenge, amezitaka halmashauri kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu na Urithishanaji Madaraka ili kuwezesha taasisi za umma kutoa huduma bora na endelevu.

Kitenge alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu na Urithishanaji Madaraka kwa Maofisa Utumishi Waandamizi wa Halmashauri za Mikoa ya Mara, Kigoma, Singida na Dodoma.

Alisema kutokana na Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2002 na Sera ya Menejimenti ya Ajira ya Mwaka 2008, waajiri katika wizara na taasisi za umma wamepewa sehemu kubwa ya majukumu ya kusimamia masuala muhimu yanayohusu watumishi wao, hivyo mpango huo ni nyenzo muhimu katika usimamizi wa watumishi.

Bila kuwa na jitihada na mipango mahususi, alisema halmashauri zinaweza kuwa na watumishi wachache wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za madaraka pindi zitakapokuwa wazi.

Kutokana na hali hiyo, alisema mipango hiyo itawezesha kusimamia rasilimali watu kwa utaratibu mzuri pamoja na kubaini mahitaji na upatikanaji wa rasilimali watu kwa wakati.

"Halmashauri zinatakiwa kuwa na watumishi wa kutosha wenye sifa na uwezo unaotakiwa mahali pa kazi ili kuleta tija na kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kutoa huduma bora kwa umma," alisisitiza. Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Rasilimali Watu TAMISEMI, Marko Masaya, aliishukuru Ofisi ya Rais-Utumishi kwa kuandaa mafunzo ambayo yatawasaidia kuandaa mipango ya rasilimali watu na urithishanaji madaraka kwa usahihi.

Masaya alimhakikishia Kaimu Katibu Mkuu, kwamba TAMISEMI ikiwa msimamizi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa watahakikisha maelekezo hayo yanatekelezwa.

Akimkaribisha Kaimu Katibu Mkuu kufungua mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi Uendelezaji Rasilimali Watu, Ofisi ya Rais - UTUMISHI, Dk. Edith Lwiza, alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa wiki moja na yanashirikisha washiriki kutoka halmashauri za sekretarieti za mikoa ya Mara, Kigoma, Singida na Dodoma.

# Waganga wamwomba askofu kuombea mvua

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAGANGA wa tiba asili katika Kijiji cha Gambosi wilayani Bariadi Mkoa wa Simiyu, wamemwomba Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, awaombee ili kupata mvua ya kutosha kwa ajili ya kilimo mwaka huu.

Waganga hao walitoa ombi hilo walipokutana na askofu huyo kuzungumza nao mambo mbalimbali ikiwamo kudumisha mila na desturi za Kisukuma, kujikinga na ugonjwa wa Uviko-19 na kupiga vita ramli chonganishi.

Mbali na ombi hilo, waganga hao pia walimwomba Askofu Sangu kuwasaidia kuwajengea ofisi katika kijiji hicho ili waweze kutambulika rasmi na kazi zao wazifanye kwenye eneo moja.

Katika mkutano huo uliofanyika kwenye viwanja vya Kanisa Katoliki Kigango cha Gamboshi, waganga hao walimwomba Askofu Sangu kufanya maombi hayo kutokana na hali ya hewa kuonyesha mvua kuchelewa kunyesha kulinganisha na miaka mingine.

"Mhashamu Baba Askofu, tunakuomba tunapoelekea msimu mpya wa kilimo utuombee kwenye kijiji chetu tuweze kupata mvua ya kutosha mwaka huu," alisema Isabile Magaja.

Naye Mwenyekiti wa waganga hao, Saguda Busaliguka, alimwomba Askofu Sangu kuwasaidia waweze kupata ofisi kijijini hapo kwa ajili ya kufanyia kazi za kwa amani, huku akieleza uwapo wa amani na upendo katika kijiji hicho.

"Watu wamekuwa wakitambua Gamboshi kama kijiji cha uchawi Tanzania, lakini jambo hilo siyo kweli, hapa ni amani na upendo, tunashukuru askofu kwa kuja hapa kisha kukutana na sisi," alisema Busaliguka.

Askofu Sangu akizungumza katika mkutano huo, aliwataka waganga hao kuwa kielelezo kikubwa kwenye jamii katika kutunza na kuenzi mila na desturi za Kisukuma.

"Kupitia kazi yenu mnayo nafasi kubwa kwenye jamii kuhimiza mila na desturi kulinda, kupiga vita mambo maovu kama mauaji ya watu wenye ualbino, mauaji ya wazee na vikongwe pamoja na utoaji wa mimba," alisema.

"Mungu ametuumba binadamu wote sawa, kuwaua albino, kutoa mimba ni kumkosea Mungu, nyie mnafanya kazi hizi kwa wema...mnatibu watu kwa miti shamba jambo jema hata kwa Mungu, lakini ni wajibu wetu kupiga vita matukio haya," alisema.

Aliwataka wakazi wa kijiji hicho pamoja na waganga wa tiba asili, kujenga utamaduni wa kupeleka watoto shule badala ya kuwafanyisha kazi za nyumbani.



Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), James Ntalika (kulia), akimwelimisha mfanyabiashara wa Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma jana, wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wajasiriamali wafundwa kukuza biashara

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAJASIRIAMALI wadogo mkoani Njombe wametakiwa kukuza biashara zao kufikia kiwango cha kuwa wawekezaji wakubwa na hatimaye kusajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Ushauri huo ulitolewa jana kwenye mafunzo ya wajasiriamali mkoani hapa na Meneja wa Kanda Nyanda za Juu Kusini wa TIC, Venance Mashiba. Alisema kupitia mafunzo hayo wanaelekeza mambo ya msingi ikiwamo kujua maeneo sahihi ya kupata msaada wa kukuza biashara.

"Tunaelekeza kama taasisi za serikali ambazo zinatoa huduma mbalimbali ambazo zinaweza kukuza biashara zao kwa maana baada ya kupata elimu wanao uwezo wa kufanya biashara zao kitaalamu zaidi, hivyo kupata faida kubwa zaidi ambazo zitawezesha kuwekeza na kukuza mtaji. Hii ni njia mojawapo ambayo watu wanaitumia kuhakikisha tunawaendeleza wajasiriamali wadogo," alisema Mashiba.

Mashiba alisema pia wajasiriamali wanakabiliwa na changamoto ya namna ya usimamizi wa biashara.

"Tuna tatizo kubwa kabisa la usimamizi wa biashara kwa maana ya elimu ya usimamizi wa biashara. Hili ni tatizo ambalo linamkuta mtu anaendesha biashara tu kwa mazoea tu lakini kuna vitu vya msingi hajavifanya. Kupitia mafunzo haya, tunakumbushana na kuelekezana wanawezaje kufanya vizuri zaidi kwenye biashara zao," alisema Mashiba.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Edward Mwakipesile, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema uwapo wa viwanda vidogo nchini ni muhimu kwa sababu vinalisha viwanda vikubwa kwa malighafi.

"Lakini pia viwanda vidogo huzalisha bidhaa kwa kutumia malighafi za ndani ya nchi kutoka sekta nyingine kama kilimo na mifugo, hivyo kuimarisha mnyororo wa thamani na kuboresha biashara za wajasiriamali," alisema Mwakipesile.

Naye mjasiriamali Roida Mng'ong'o alisema wajasiriamali mkoani Njombe wanakabiliwa na changamoto ya mitaji.

"Kweli katika uwekezaji sisi wajasiriamali mkwamo upo kwenye mitaji pamoja na masoko kwa sababu vigezo ni vingi. Kwenye masoko pia hatujafikia viwango vya ubora," alisema Mng'ong'o.

## Ma-DED waagizwa kuchangisha mil. 200/- ujenzi sekondari mkoa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

WAKURUGENZI wa halmashauri mkoani hapa wameagizwa ifikapo Novemba 7, mwaka huu, wawe wamekamilisha mchango wa Sh. milioni 30 ili kupata Sh. milioni 200 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana ya kidato cha kwanza hadi cha sita ya mkoa wa Songwe.

Ujenzi wa shule hiyo ni matokeo ya agizo la Rais Samia Hassan Suluhu alilolitoa mwaka 2018 alipofanya ziara ya kikazi mkoani hapa wakati huo alikuwa Makamu wa Rais. Aliagiza mkoa kujenga shule ya kitaifa ya wasichana ili kukabiliana na idadi kubwa ya wanafunzi wa kike wanaokatisha masomo kutokana na mazingira magumu ya kujifunzia.

Katibu Tawala Mkoa wa Songwe, Misaile Mussa, alitoa agizo hilo alipokutana na wakurugenzi wa halmashauri, makatibu tawala na kamati za ulinzi na usalama za wilaya zote za mkoa ili kujadili namna ya kupata Sh. milioni 200 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa shule hiyo inayojengwa katika eneo la Myunga, wilayani Momba.

"Nataka hadi kufikia Novemba 7, kila halmashauri iwe imekamilisha mchango wake wa Sh. milioni 30 ili tumalizie hatua ya awali ya ujenzi wa miundombinu ya msingi ili wanafunzi waanze masomo kama ilivyotarajiwa, " alisema.

Awali, akisoma taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa shule hiyo, Ofisa Elimu Mkoa wa Songwe, Juma Kaponda, alisema lengo la ujenzi katika awamu ya kwanza ni ukamilishaji wa majengo ya msingi ili shule ifunguliwe.

Alisema shule hiyo ya wasichana itakuwa ya kidato cha kwanza hadi cha sita na inatarajia kuchukua wanafunzi 6,340.

Kaponda alisema hadi kukamilika kwake shule hiyo itagharimu Sh. bilioni 3.4 na kwamba fedha hizo ni pamoja na michango ya wadau mbalimbali wa elimu mkoani hapa.

# Magu yapata bil. 2.4/- ujenzi wa madarasa

**Na Anthony Gervas,** MAGU

SERIKALI imetoa shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za sekondari na msingi katika kata mbalimbali wilayani Magu mkoani Mwanza.

Hayo yamesemwa jana mjini Magu na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mpandalume Simon, katika kikao cha mapendekezo ya awamu ya pili ya kuanzishwa Wilaya na Halmashauri mpya ya Kisesa.

"Halmashauri yetu ya Wilaya tumepokea Sh. bilioni 2.4 kutoka serikalini kwa ajili ya miradi ya elimu, lengo ni kuondoa kero za upungufu wa vyumba vya madarasa katika kata zetu," alisema Simon.

Alisema haijawahi kutokea serikali kutoa fedha nyingi kama hizo katika miradi ya elimu, hivyo wana sababu za kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwakumbuka katika suala zima la elimu.

Simon aliwataka watendaji wa serikali na kata kuhakikisha wanasimamia vizuri fedha hizo ili ziweze kutumika katika miradi iliyolengwa, huku akiwaonya kuacha matumizi mabaya ya fedha hizo.

Katika kikao hicho, madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo walipendekeza kugawanywa kwa wilaya hiyo na kuanzishwa mpya ya Kisesa, ambayo itaundwa kutokana na tarafa mbili za Sanjo na Kahangara.

Diwani wa Kisesa, Marco Kabadi, alisema kuwa hawana shaka kuanzishwa Wilaya na Halmashauri mpya ya Kisesa, kwani ni jambo zuri, huku akipendekeza na mpaka wake.

Madiwani hao na wajumbe wengine waliunga mkono mapendekezo hayo na mipaka yake, ambayo yatazingatia vigezo vya serikali, vinavyotaka wilaya mpya angalau iwe na idadi ya watu wasiopungua 200,000 na wilaya kongwe ibaki na idadi ya watu wasiopungua 300,000.

Moja ya vigezo vingine vilivyotajwa katika rasimu ya mapendekezo hayo ni pamoja na huduma muhimu kama vile kuwepo maeneo ya biashara, viwanda vikubwa na vidogo, vituo vya afya, shule, miundombinu ya barabara pamoja na masoko.

Walisema vigezo vingine ni huduma za kibenki na kifedha, maji, mpango wa matumizi bora ya ardhi usiopungua asilimia 75 pamoja na vyuo vikiwamo vya ufundi.

# Ruvuma yachanja 44,000 UVIKO-19

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKOA wa Ruvuma umemaliza chanjo ya kwanza ya UVIKO-19 kwa kuchanja watu 44,000.

Hayo ylisemwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, aliyewakilishwa na Dk. Yona Mwakabumbe kwenye sherehe za Maulid zilizofanyika Msikiti wa Wilaya katika Manispaa ya Songea, ambapo mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge.

Alisema idadi ya waliochanja ni kuanzia Agosti 4 hadi Oktoba 15, mwaka huu ambapo Mkoa umefanikiwa kumaliza chanjo zote na za ziada aina ya Jonson&Jonson ambazo mkoa ulipewa.

Aliwapongeza waumini wa Kiislamu kwa kutoa ushirikiano mkubwa wakati wa kutekeleza zoezi la chanjo ya kwanza, ambapo alisema wataalamu wa afya walikaribishwa kutoa elimu na fursa ya kuchanja waumini.

"Baada ya kumaliza chanjo ya kwanza, serikali imetoa chanjo ya pili aina ya Sinofam, Mkoa wa Ruvuma tumepata mgao... ni chanjo salama unachoma na kurudia baada ya siku 28," alisisitiza Dk. Kanga.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi, Katibu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Ruvuma, Rajabu Mustapher Songambele, alisema MASJD NUR katika Manispaa ya Songea imetenga hekari 80 kwa ajili ya kujenga shule ambayo itatoa elimu kuanzia chekechea hadi sekondari.

"MASJD NUR imekusudia kuwekeza kwenye elimu ili watoto wetu wapate elimu bora na kuwa katika misingi na maadili mema kwa sababu jamii hivi sasa imepoteza maadili," alisisitiza Songambele.

Kwa upande wake, Brigedia Jenerali Ibuge aliwapongeza waumini wa Kiislamu kwa maamuzi ya kujenga shule na kituo cha afya na kusisitiza kuwa kwa kufanya hivyo wanaisaidia serikali kuwapatia Watanzania elimu na afya.

Alisema Mkoa unawaunga mkono katika utekelezaji wa miradi hiyo, ingawa alitaka kuwapo uwazi kuhusu shughuli hizo zitavyofanyika ikiwamo kujua fedha zilizoingia na matumizi yake.




Mkuu wa Huduma za Wateja Rejareja na Wajasiriamali wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo (katikati) na wafanyakazi wengine wa benki hiyo wakionyesha ufunguo wa gari aina ya Toyota Vanguard (inayoonekana nyuma) itakayotolewa kwa mshindi wa kampeni mpya ya benki hiyo inayofahamika 'Weka Mkwanja Tukutoe! wakati wa unzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EXIM sasa yaja na mkakati kuhamasisha uwekaji akiba

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imezindua kampeni ya 'Weka Mkwanja Tukutoe!' Inayolenga kuhamasisha Watanzania kujiwekea amana, huku wakipata fursa za kunyakua zawadi mbalimbali ikiwamo fedha taslimu pamoja na gari aina Toyota Vanguard.

Kampeni hiyo ya miezi mitatu inayofahamika kama 'Weka Mkwanja Tukutoe!' Ilizinduliwa jana jijini Dar es Salaam na imepangwa kuwafikia Watanzania wote wakiwamo wateja wa benki hiyo pamoja na wale watarajiwa.

Akizungumza wakati hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo, Mkuu wa Huduma ya Wateja Rejareja na Wajasiriamali wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo, alisema kampeni hiyo inalenga kuleta mabadiliko kwenye mtazamo wa uhifadhi wa amana miongoni mwa Watanzania kutoka kuhifadhi pesa majumbani na badala yake wazihifadhi kupitia benki hiyo kwa usalama wa fedha zao sambamba na faida nyingine nyingi ikiwamo riba.

"Lengo si tu kuhamasisha Watanzania kujenga utamaduni wa kujiwekea amana, tunachohitaji ni kuona kwamba Watanzania wengi wanajiwekea amana zao sehemu salama ili kujiendeleza kukua kiuchumi ndio maana tumejipanga kuwahamasisha watumie akaunti zetu mbalimbali ikiwamo akaunti ya mshahara inayotumika kwa matumizi mbalimbali ya kila siku."

"Nyingine ni akaunti ya mzalendo inaendeshwa bila makato ya kila mwezi, akaunti ya haba na haba, akaunti ya faida hizi zinakuruhusu kuweka akiba na kupata riba, tuna akaunti ya Nyota ambayo ni akaunti maalum kwa ajili ya kuwawekea watoto akiba ya baadaye na mwisho kabisa tuna akaunti ya wajasiriamali inayowahudumia wafanyabiashara na mahitaji yao tofauti tofauti ya kibiashara," alisema Lyimo.

Akitaja zawadi zikazotolewa kupitia akaunti hiyo, Lyimo alisema ni pamoja na zawadi za fedha taslimu kiasi cha Sh. milioni 1, kwa mwezi na kila mwezi kutakuwa na washindi sita, sambamba na kuingia kwenye droo itakayowawezesha kushinda zawadi kubwa ya gari aina ya Toyota Vanguard.

"Hivyo basi wateja wetu wa sasa na wale wapya watakuwa kwenye nafasi ya kujishindia zawadi hizi kila wakapojiwekea akiba ya kuanzi shilingi 500,000 na kuendelea. Kadili wanavyojiwekea amana kubwa zaidi ndivyo wanavyojiweka kwenye nafasi ya kushinda zawadi kubwa zaidi," alifafanua.

# Mkenda afuatilia mbolea ya Burundi

**Na Mwandishi Wetu,** BUJUMBURA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, ametembelea na kufanya mazungumzo na menejimenti ya kiwanda cha mbolea cha FOMI ambacho kupitia kampuni yake ya ITRACOM imeanza ujenzi wa kiwanda cha mbolea jijini Dodoma.

Katika ziara hiyo Waziri Mkenda pamoja na wataalamu mbalimbali aliombatana nao, alikagua kiwanda cha FOMI na kuona kinavyofanya kazi lengo likiwa kuona uwezekano wa kiwanda hicho kama kinaweza kuuza mbolea yake Tanzania kwa bei nafuu kwa wakulima na kupatikana kwa wingi na kwa wakati.

Prof. Mkenda alisema kuwa kiwanda hicho nchini Burundi kinazalisha tani kati ya 120,000 mpaka 150,000 kwa mwaka kulingana na soko la mbolea huku kikiwa kimeanza ujenzi wa kiwanda cha kisasa jijini Dodoma ambapo kitapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha Tani 600,000 za mbolea ambazo ni zaidi ya mahitaji ya mbolea nchini ambayo ni kati ya tani 400,000 mpaka 500,000 kwa mwaka.

Alisema kuwa wakati serikali inaendelea na mkakati wa ujenzi wa kiwanda kikubwa cha mbolea Tanzania, vilevile inaendelea na mkakati wa kuhakikisha kuwa inatafuta mbolea inayoweza kupatikana kwa wakati na kuwafikia wakulima kwa bei nafuu.

Waziri Mkenda alimhakikishia Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Ntirampeba Simon, kuwa serikali ya Tanzania itakuwa bega kwa bega kuhakikisha kuwa ujenzi wa kiwanda hicho unakamilika kwa wakati uliokusudiwa.

"Wawekezaji wote wanaowekeza kwenye biashara ya pembejeo Tanzania tunawahakikishia kuwa Tanzania ni nchi salama kwa uwekezaji hivyo wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kuwekeza," alisema Waziri Mkenda.

Kwa upande wake Waziri wa Mazingira, Kilimo na Uvuvi wa Burundi, Dk. Rurema Deo-Guide, alisema kuwa mazungumzo hayo yamekuja wakati mwafaka kwani yameongeza wigo mpana zaidi kwa kubadilishana mawazo katika sekta ya kilimo.

Dk. Rurema alisisitiza kuwa katika muktadha wa kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo kuna mambo muhimu mawili ya kuzingatia ambayo ni maji, ardhi na mbolea na Burundi sekta ya mbolea imeimarika na uzalishaji unatosheleza mahitaji ya wakulima.

Simon alisema kuwa menejimenti ya kiwanda hicho imeendelea kufurahishwa sana kwa ushirikiano unaoonyesha wa viongozi wakuu wa Tanzania kwa kutembelea Burundi mara kwa mara husasani kukitambua na kukithamini kiwanda hicho.

Alisema kuwa mbolea inayozalishwa kiwanda hapo ni nzuri na inayohimili hali yoyote ya hewa na ardhi kwa mujibu wa utafiti walioufanya.

Awali Prof. Mkenda alikutana na kufanya mazungumzo na wafanyakazi wa Ubalozi wa Tanzania nchini Burundi ambapo aliwapongeza kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya, huku akiwasihi kuhakikisha kuwa wanaendeleza ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.

Kaimu Balozi wa Tanzania nchini Burundi, Salvatory Mbilinyi, alimhakikishia Waziri Mkenda kuwa ubalozi unaendelea kuwa kiungo muhimu katika juhudi za serikali ya Tanzania za kuhakikisha Burundi kama nchi jirani inaendelea kuwa na amani.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Nguzo Mbili, wilayani Geita, Tunu Mjema (wapili kulia), akipokea kikombe cha ushindi kutoka Ofisa Elimu Mkoa wa Geita, Masumbuko Stephano, baada ya shule hiyo kuibuka mshindi wa jumla katika shindano la kuchora mchoro wa usalama barabarani linaloendeshwa na kampuni ya Puma Energy, kupitia programu yake ya kutoa mafunzo ya elimu ya usalama barabarani kwa kushirikiana na Shirika la Amend, ambapo shule tano za mkoa huo, zilishiriki. Watatu kulia ni Ofisa Usalama na Mazingira wa Puma Energy, Ambokege Minga.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yawataka wanawake kuvichangamkia viwanda

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba, amewataka wanawake nchini kuchangamkia fursa za kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ili kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Mwenyekiti huyo alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua Wiki ya Kongamano la Wanawake wa Kanisa la Mlima wa Moto (WOCA 2021) lenye lengo la kutoa elimu kwa wanawake kuhusu afya, elimu, uchumi, uhusiano, malezi na fursa mbalimbali.

Alisema asilimia kubwa ya bidhaa zinazozalishwa viwandani duniani kote, wateja wakuu ni wanawake hivyo ipo haja na fursa kuanzisha viwanda kwa ajili ya kujinufaisha.

"Tulikuwa na viwanda mbalimbali nchini wakati wa Hayati Mwalimu Julius Nyerere, vingi vikafa ni muhimu wanawake tukaamka wakati huu wa kuinua uchumi tukaanzisha na sisi viwanda vyetu mfano vya kuzalisha vitenge na kanga kubwa zinazotutosha kwa sababu kanga nyingi zinazozalishwa na ndogo hatuwezi kuzifunga zikakaa kiunoni," alisema Kamba.

Naye Mchungaji Kiongozi wa Kanisa hilo, Bishop Rose Mgeta, alisema kongamano hilo lililoanza Jumapili iliyopita linatoa fursa kwa wanawake wote kujifunza kuhusu sheria za fedha na malezi ya watoto.

"Tunaamini mwanamke akipewa nafasi anaweza kufanya mambo makubwa na ndio maana tumekuja na kongamano hili kubwa la WOCA linaloshirikisha wanawake wa kanisa hili na kutoka maeneo yote kuja kujifunza bure," alisema Bishop Mgeta.

Alisema kongamano hilo lina kauli mbiu inayosema, 'Wajibu wa mwanamke katika ujenzi wa kanisa, uchumi na familia bora (WOCA 2021)'.

Naye Mlezi wa Wanawake wa kanisa hilo, Mchungaji Rose Rwakatare, alisema kongamano hilo litamfanya mwanamke kujitambua na kuwa na uchumi wake.

"Mama ndio kila kitu kwenye familia. Wanawake tunaendeleza kazi iliyoachwa na marehemu Dk. Getrude Rwakatare na tunaendelea kuyafanyia kazi maono yake kuhakikisha wanawake wanafanya mambo makubwa ndani ya jamii zetu na kushika uchumi wa nchi," alisema Mchungaji Rose.

# NFRA sasa yanunua mahindi yote Rukwa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

SERIKALI kupitia Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) imenunua mahindi yote ya wakulima wadogo katika mkoa wa Rukwa tani 21,500.

Meneja wa NFRA mkoani Rukwa, Marwa Range, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na mwandishi wa habari hizi aliyetaka kujua ni tani ngapi ambazo zimenunuliwa kutoka kwa wakulima mpaka sasa.

Alisema kuwa wakulima wadogo hasa wa vijijini wameuza mahindi yao, hivi sasa wanaoendelea kuuza mahindi ni wafanyabiashara na tayari zimenunuliwa tani 21,500 na lengo ni kununua tani 30,000.

Range alisema kuwa NFRA iliamua kuongeza vituo vya ununuzi wa mahindi ambapo mkoa wa Rukwa ulikua na vituo 15 katika wilaya mbalimbali kitendo kilicho wezesha wakulima kuuza mahindi yao bila usumbufu.

Mmoja wa wakulima wa Kijiji cha Ntatumbila wilayani Nkasi, Maria Kayanda, alisema kuwa wanaishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuongeza fedha kiasi cha Sh. bilioni 50 ambazo zimewezesha kununua mahindi yao.

Naye Mussa Katanta mkulima wa Kijiji cha Milepa wilayani Sumbawanga, alisema kuwa hifadhi mwaka huu serikali imewakomboa wakulima wadogo kwani wameweza kuuza mahindi yao na wako tayari kwa msimu mpya wa kilimo kwani wana fedha za kununulia pembejeo za kilimo.

ama
ALHAMISI OKTOBA 21, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Watumia ARV washtukia kupotoshwa tiba UVIKO 19 inayoendelea haiwahusu**



Ukurasa 12

**Zifahamu sababu kuu, pia nchi watu wanakoishi miaka mingi**

# Darasa la mazingira na nyenzo sita zinazobadili hali ya hewa



Wakulima wa mpunga wakiwa shambani nchini, zao linalotajwa kuchangia ongezeko la joto duniani. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA hali ya hewa kipo kinachoitwa tabianchi. Kimsingi ni hali ya mabadiliko kwenye hali ya hewa, kwa maana ya joto, baridi upepo unaovuma na mvua inayojirudia kwa muda mrefu.

Namna mtu anaweza kukabili hali hiyo, ni sehemu ya magumu anayokutana nayo mwanadamu. Wataalamu sayansi wameorodhesha hatua na njia zinazofaa kutumika kukabili hali hiyo hasi.

KUELIMISHA WASICHANA

Kuna uboreshwaji elimu kote duniani kwa hatua inayozama zaidi kuwaelimisha wasichana, hata ikawasaidia kupambana na mabadiliko chanya ya hali ya hewa.

Nini sababu? Wasichana wanatajwa wanapata watoto mapema zaidi na baadhi yao wakiwa masomoni. Inaelezwa, iwapo mabinti watasoma hadi ngazi ya sekondari, itakabili hali hiyo na hata kuwapo matarajio ya kitaalamu ifikapo mwaka 2050, watu milioni 840 duniani watapungua.

Inafafanuliwa, kuwaelimisha wasichana ni zaidi ya idadi ya watu duniani. Wanawake wanashiriki katika kazi, biashara na siasa, vyote vikiwa na nafasi ya kuzuia mabadiliko hasi ya hali ya hewa.

Inaelezwa, kuwaweka wanawake zaidi katika usimamizi kunachangia kuwapo sera bora inayohusu mabadiliko ya hali ya hewa, kwani ni wasikilizaji bora wa ushauri sayansi, kama ilivyodhihirika kwenye matuko kadhaa, ikiwamo corona.

**ULIVYO MMEA MUANZI**

Muanzi una kawaida ya kukua haraka zaidi duniani hadi kufikia kimo cha mita moja na inachukua hewa ya kaboni au ukaa kwa haraka kuliko miti, pia migumu, hali inayosaidia kutengeneza fenicha za ujenzi.

Kuna mfano wa kuupanda mmea muanzi unavyostahimili wadudu na kuboresha udongo kuzuia mmomonyoko, huku ukipunguza hatari ya mafuriko.

Mfano nchini Indonesia kuna mimea mahsusi ya kupunguza gesi ya kaboni imepandwa katika vijiji 1000. Matarajio ni kila kijiji kuzungukwa na kilomita 20 za mraba za msitu wa bamboo, mimea ya chakula na mifugo. Sasa wanataka kupeleka wazo hilo katika nchi nyinginezo tisa.

**SHERIA ZA MAZINGIRA**

Kwa kutumia sheria ya kupambana na uchafuzi wa mazingira, inatajwa ni silaha zenye nguvu zaidi kuwakabili wachafuzi wa mazingira, kutoka taasisi au vyanzo vinginevyo, vikiwamo vya umma.

Hivi karibuni nchini Uholanzi kwa kutumia mwongozo wa Makubaliano ya Hali ya Hewa ya Paris ya mwaka 2014, kampuni ya mafuta ya Shell iliamuriwa kupunguza gesi chafu,

Pia, hata wanasheria wamekuwa wabunifu kukitumia sheria za haki za binadamu, ajira na hata za kampuni, kujihami na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Mwaka 2020, kikundi cha wawekezaji chenye hisa za thamani ya dola 35 (Sh.77, 000) tu kilifanikiwa kuzuia kiwanda cha mkaa wa mawe kujengwa nchini Poland, kwa kutumia nguvu ya haki za hisa zake ndani ya kampuni ya nishati nchini Poland na mahakama ikaiamuru kufungua kiwanda kipya cha mkaa wa mawe ilikuwa biashara mbaya iliyoku kinyume na sheria.

**MAJOKOFU YA GESI**

Kila jokovu na kiyoyozi huwa na kemikali na baadhi ya mazao yana hali mbaya zaidi kimazingira na atahri kwa jamii. Mwaka 2017, viongozi wa dunia walikubaliana kumaliza baadhi ya athari mbaya zaidi.

**USAFIRI WA MELI**

Sekta ya usafiri wa baharini inaelezwa kuwa muhimu sana kwa uchumi duniani na asilimia 90 ya biashara ya sekta hupitia baharini, Ni sekta inayochangia asilimia mbili ya gesi chafu, huku idadi ikitarajiwa kuongezeka ndani ya miongo inayokuja.

Vyombo vidogo vya usafiri majini, navyo hutumia asilimia 25 zaidi ya mafuta ya dizeli chafu, ikilinganishwa na meli zinazoteleza.

Ili kupunguza gesi ya carbon inayosababishwa na viumbe hawa wa baharini, wataalamu wamebuni njia kuzifanya meli kuteleza zaidi.

**KUBUNI MCHELE MPYA**

Mchele unazalisha kiwango sawa cha hewa kaboni, sawa na inayotoka katika sekta ya usafiri wa angani, hasa inapopandwa kwenye maeneo yanayofurika maji kuzuia magugu.

Pia, maji hayo huzuia oksijeni kufika kwenye udongo na kuchangia kuwapo mazingira bora kwa bakteria zinazozalisha gesi ya methane, ambayo kwa kiwango cha kilo moja, inasababisha joto kuongezeka mara 25, kuliko hewa kaboni au ukaa kwa jina lingine.

Kukabili athari hizo, wanasayansi wanafanya mabadiliko katika kilimo cha mchele kwa kubuni mbegu tofauti zinazoweza kukua kwenye mashamba ya kawaida, ikitarajiwa mageuzi makubwa katika miaka 10 ijayo.

• **Kwa mujibu wa BBC.**

AFYA

# Namna ugumu kuvaa barakoa ndani ya madarasa kila aina

## • Dhana uelewa duni yatawala kote

**Na Mary Geofrey**

LEO mtu anapohoji barakoa ni nini? Pasipo shaka, jibu lake nikile walimu shulenihufanya masihara kwa wanafunzi 'swali rahisi kwa mjinga.'

Mtu akihoji kazi yake nini? Watakaokosa ni wengi,si ajabu majibu kuangukia kukabili corona pekee.

Ni kweli, barakoa inahamasisha vita kukabili maambukizi ya UVIKO-19 duniani, lakini upande wa ujasiriamali nako si haba, ina fursa.

Kitaalamu ni kifaa tiba ambacho kabla ya mlipuko, ilihudumia afya na kuuzwa kwenye maduka muhimu ya dawa za binadamu na mifugo pekee, wataalamu wajikinge.

Leo hii, uuzaji sasa umeenea penye mikusanyiko ya watu kama sokoni, stendi za mabasi, nyumba za ibada, shuleni, viwandani na sokoni.

Pia, kuna ofisi za umma na binafsi, barakoa huuzwa hadi getini kwa walinzi kuwasaidia waliosahau watimize sharti la kuvaa kabla ya kuingia.



Watu wakijihami dhidi ya UVIKO 19. Ukurasa 13 uvaaji barakoa. **PICHA ZOTE: MARY GEOFREY.**

### UMUHIMU WAKE

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Elimu kwa Umma wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Ama Kasangala,anaelezea kazi ya barakoa ni kupunguza uwezekano wa virusi kupitia mate au maji wanapoongea, kukohoa au chafya kutoka aliyeambukizwa hadi kwa mwingine.

Barakoa hufyonza maji ya mwathirika, kabla ya kusambaa na kuambukiza mwingine. Kitaalamu inatajwa mtu mmoja kati ya sita walioambukizwa virusi corona hawaonyeshi dalili.

### FURSA ZA KIUCHUMI

Wakati serikali inapigia debe uvaaji barakoa kujikinga na maambukizi, wajasiriamali wanatumia fursa hiyo kunasa vipato vitokanavyo na mauzo yake.

Uchunguzi wa Nipashe kwa kushirikiana na wadau, taasisi ya Chimbua Communication, ,Mkoa wa Dar es Salaam, umebaini wafanyabiashara wadogo wameenea penye mikusanyiko, wakiwahamasisha wahitaji"usipovaa barakoa hakuna kuingia, wala kupata huduma."

Hassan Hafidh (19), muuza barakoa nje ya makao makuu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), katikati ya jijiDar es Salaam, anafafanua hununua mzigo kwa Sh. 5,000 na inampa faida Sh.20,000 anapomaliza, bei kila moja Sh. 500 ingawa analalamika,biashara imepungua sasa.

Mjasiriamali huyo, mhitimu wa mafunzo ya udereva Daraja D, anakiri inamsaidia kipato cha kukataleseni, ahamie kwenye fani yake aendeshe magari.

"Tangu nimeanza kazi hii Januari, nimeshakusanya Sh. 90,000, bado Sh. 60,000 nikalipie leseni," anasema Hafidh, anayefafanua anauza barakoa za aina zote, ingawa analaamika licha ya kupata kati ya Sh. 10,000 hadi Sh. 20,000 kwa siku, lakini wateja wanapungua.

Nje ya hospitali Muhimbili na taasisi zake, kuna wafanyabiashara walioshamiri na barakoa mkononi,nyingine zimening'inizwa vibandani, kwa bei kati ya Sh.500 na Sh.1, 000 kulingana na ubora, kuhudumia kinga dhidi ya maambukizi ya UVIKO-19.

Mwanamama Swaumu Makubi, anaeleza licha ya wanaoingia getini wanaweza kupita bila kuvaa barakoa, wamekuwa wakiwatisha, hawaruhusiwi kuingia eneo hilo bila barakoa.

"Tunajipatia riziki dada yangu, pia tunaisaidia serikali katika kuhakikisha watu wanaoingia hapa Muhimbili wanavaa barakoa ili kujikinga na kuwakinga wengine na maambukizi,"anasema.

Hamis Mwijuma, anafafanua hoja hiyo, akisema kuna watu wapya kila siku wanaoingia hospitalini, hata kuwawezesha kuuza wastani wa barakoa 50 kwa siku, kila moja Sh. 500.

Mlinzi geti (jina tunalihifadhi), anasema wamekuwa wakihimiza kila anayeingia avae barakoa, lakini kwa sababu ya wingi wao, kuna wakati baadhi wanapita bila ya kuvaa. "Siyo wengi wanaopita bila kuvaa barakoa.Inatokea bahati mbaya unakuta tumezidiwa na watu wanaingia na kutoka,lakini ni lazima tukague,"anasisitiza.



Wauza barakoa wakiendelea na majukumu.

### MUHIMBILI INAVYOKABILI

Nipashe liliingia hadi hospitalini Muhimbili, ikishuhudiawanaotembea wamevua barakoa, wapo waliozishusha kidevuni, wengine wamezishikilia wakisubiri pa kutolewa huduma ndio wavae.

Mgonjwa Emmanuel Mhagama, anajitetea anapotembea peke yake si hatari, isipokuwa anapoingia kwa daktari ndio anavaa, akiamini anafuata masharti.

Mgonjwa Mary Chuala, anasema barakoa inamsaidia kujikinga penye mikusanyiko na anapokuwa peke yake anavua kupumua vizuri.

Mkuu wa Mawasiliano wa hospitalini Muhimbili, Aminiel Aligaesha, anasema umeshawekwa mwongozo kutoruhusu mtu kumuona daktari bila ya kuvaa barakoa.

Anasema:"Sisi tumeshatoa maagizo kuwa hakuna mgonjwa anayeingia kwa daktari bila kuvaa barakoa kwa hiyo hatuwezi kuanza kukamata mtu mmoja mmoja kulazimisha wazivae."

### STENDI YA BASI?

Katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, jijini Dar es Salaam, nako Nipashe ilishuhudia mwingiliano mkubwa wa watu, kuwapo haraka za abiria kuwahi usafiri hasa asubuhi, zinavyowafanya wasizingatie uvaaji barakoa, zikibaki mikononi.

Vaileth Shirima,mjasiriamali muuza barakoa nje ya kituo hicho, anasema wako wenzao wa Muhimbili, huwashawishi wateja kuingia kituoni wamevaa barakoa.

"Kazi yetu tunawaambia kabisa kituoni 'huingii bila barakoa'kuhusu kama wanavaa au hawavai, hilo ni jambo lingine," anadokeza.

Meneja Uhusiano na Ufuatiliaji wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Maira Mkama, anakiri wauzaji nje ya kituo wanajitahidi kuhamasisha uvaaji barakoa, lakini wengi huzivua wanapoingia kituoni zikibaki mkononi, jambo lililo nje ya uwezo wao. Hata hivyo, wanaendelea kuelimisha, ikiwamo matangazo.

Bakari Kisiga, dereva wa teksi wa eneo hilo anaungana na wajasiriamali, akikiri uvaaji barakoa eneo hilo ni kidogo, wengi wana haraka zao kuwahi mabasi.

### VIONGOZI WATENGENEZAJI

Fundi nguo, Joyce Mosha, anasema anashona barakoa na kuziuza Sh. 1,000, akitumia vitambaa vizito kama kitenge na batiki, pia kuna vyepesi aina ya tetroni kinachokaa ndani kupata barakoa salama,

Pia, anataka kitambaa aina 'scuba kinachojitegemea, pasipo kuchanganya na chepesi.Je, alifahamu vipi kutengeneza? Joyce anafafanua:

"Nilijifunza kushona barakoa kwa kujijaribisha mwenyewe, nilishona kitenge chenyewe kilichokunjwa mara mbili, lakini nikagundua siwezi kupumua vizuri. Ikabidi nishone upande mmoja na kuchanganya na tetroni. Elimu hii niliipata kwa njia ya vyombo vya habari."

Fundi Robert Joel, anaeleza anavyoshona na kuuza barakoa kulingana na mfano anaoufuatilia, bidhaa zake akiuza kati ya Sh.1, 500 na Sh. 2,000, kulingana na aina na hitaji la wateja, watu binafsi, pia kampuni na hasazinazoshonea wafanyakazi.

"Huwa sibuni, kwa sababu barakoa zipo za aina nyingi. Huwa napenda mteja aje na mfano wa barakoa anayotaka nimshonee," anasema Robert.

### TMDA NA VIWANGO BORA

Ofisa Ukaguzi wa Maabara ya Mikrobaiolojia wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Obson Julius, anasema zaidi ya asilimia 90 ya barakoa zinazozalishwa mtaani zinatumia khanga, vitenge na vitambaa salama.

Anasema barakoa zinazozalishwa na wajasiriamali zimefanyiwa vipimo na maabara zao na kubainika zina uwezo hadi asilimia 99 kukinga maambukizi ya bakteria wanaoambukiza kwa UVIKO-19.

Julius anataja yanayongaliwa ka-

Inaendelea Uk. 13

AFYA

# ...Watumia ARV washtukia kupotoshwa tiba UVIKO 19 inayoendelea haiwahusu

## • Daktari bingwa: Kila moja inajitegemea
## • Waliougua: Tuko wachache, tumetibiwa

**Na Beatrice Shayo**



"KUTUMIA dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI (ARV) kwa kufuata mpangilio haina maana kuwa niache kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa UVIKO-19. Wapo wanaodhani hatuwezi kuupata huo ugonjwa, jambo ambalo siyo kweli," anatamka George Mbogo (55), anayejitambulisha kuishi na virusi vya UKIMWI.

Anasema upotoshaji unaoendelea unawaweka wengi hatarini kuamini wanatumia ARV, ambazo kazi yake ni kuimarisha kinga mwilini na hawawezi kupata UVIKO-19.

"Ukiwa mfuasi mzuri wa dawa, ina maana kinga zako zitaimarika na kama zikiimarika hautaweza kupata misukosuko ya magonjwa ya kuambukiza.

"Watu wamechukulia fursa hiyo, kwa sababu ni mfuasi mzuri wa dawa anakuwa amesimama vizuri na ina maana kinga yake ipo juu, dhidi ya maambukzi ya corona,: anasema.

Mbogo anafafanua wanaotumia ARV na wasiotumia, kwa ujumla wapo hatarini kupata ugonjwa wa UVIKO-19.

**JITIHADA SERIKALINI**

Mbogo, ambaye ni mjasiriamali na amekuwa akitoa huduma za afya ngazi ya Jamii (CHW), anasema kitendo cha serikali kuwapa dawa za miezi sita, imewasaidia kuondoa msongamano katika vituo vya afya wanakoenda kuchukua dawa, tangu kuzuka maradhi UVIKO 19.

Anasema ni hatua inayowapa uhuru kufanya shughuli nyingine kama kusafiri kwenda mikoa mwingine na kufanya biasahara muda mrefu, wakarejea kuchukua dawa.

"Awali kabla ya UVIKO-19 kuingia tulikuwa tunapewa dawa za mwezi mmoja, ukiendelea vizuri unapewa dawa za miezi miwili mpaka miezi mitatu," anasema Mbogo akifafanua Uviko-19 ilivyoingia serikali imewaongezea hadi miezi sita, kuondoa foleni katika vituo vya afya kufuata ARV.

"Unapomzungumzia mtu mwenye ugonjwa wa VVU yupo katika hatari ya kupata UVIKO-19 huu utaratibu umesaidia kwa sababu hakuna foleni, ukifika unapewa na dawa na kuondoka awali tunakutana wengi na kujikuta foleni kubwa," anaeleza

**AFANIKIWA KUJIUGUZA**

Serafika Erick (Sio jina halisi) anayeishi na VVU, anasema amewashuhudia watu wawili wanaotumia ARV wamepata UVIKO -19 na sasa afya zao ni nzuri, baada ya kupata tiba sahihi.

Anasema yupo kwenye kundi la kuwafuatilia waliokuwa wanatumia dawa za ARV kwa wakati licha ya kwamba wamepata ugonjwa huo.

"Baba yangu anatumia ARV vizuri na amekuwa akifuatilia masharti yote yanayotakiwa, lakini alipata corona na amefuatilia masharti ya ugonjwa huo na kwa sasa, anaendelea vizuri," anasema.

Hata hivyo, anakiri kutumia fursa ya kuratibu wagonjwa katika kituo cha afya, kwamba kuna wachache wenye VVU wanaoumwa UVIKO-19.

"Tangu corona iingie nina ripoti ya watu wawili. Kundi kubwa halikupata corona. Hii ni kwa sababu ni wafuasi wazuri wa matumizi ya dawa kwa hiyo magonjwa nyemelezi hayawezi kuwapata," anaeleza.

Pia, anatoa tathmini vifo vingi si vya wenye VVU, kwa sababu wana kinga dhidi ya magonjwa nyemelezi, wanapata dawa na wamewekewa mazingira bora wanafika katika kituo cha afya mara mbili pekee kwa mwaka.

**ALIYEPATWA ASIMULIA**

Daniel John (sio jina halisi), ni mtoa huduma katika kituo cha afya kimojawapo cha Dar es Salaam, anasema alipatwa UVIKO-19 Machi, mwaka huu, dalili ya kwanza ni kusikia homa usiku.

Anajitambulisha ni mtumiaji bora wa ARV na hajawahi kukiuka masharti ya matumizi. Anafafanua: "Kipindi cha wiki moja nilijikuta napata homa za usiku nikawa naendelea kwenda kazini.

"wiki iliyofuata nikiwa njiani narudi nyumbani, nikajikuta nipo kwenye daladala nashindwa kupumua, nikapelekwa hospitali nikafanyiwa vipimo nikajikuta na UVIKO-19,"

Anaeleza alitibiwa mwezi huo na akarejea hali ya kawaida, sasa akizingatia kujikinga na ugonjwa huo kwa kufuata masharti ya kuvaa barakoa, kunawa mikono kila wakati na kuepuka mikusanyiko ya watu.

**UTAFITI UNASEMAJE?**

Daktari Bingwa wa Kitengo cha Magonjwa ya Kuambukiza katika, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Pamela Kaaya. anasema hadi sasa hakuna utafiti unaonyesha anayetumia ARV haambuikizwi UVIKO-19 na kitaalamu haijajulikana kiwango anachopata hatari ya corona.

"Haisemekani kwamba mtu anayetumia ARV vizuri, inamsaidia yeye asipate corona. Hili siyo kweli 'risk' (hatari), ipo palepale kama mtu mwingine ambaye hana HIV ni hivyo hivyo," anafafanua.

"Hata kama akichanjwa, asilimia 68 ya kupata maambukizi ya corona yapo palepale na asilimia 100 ya kuzuia asife ipo pale pale," anaeleza Dk. Pamela.

Anasisitiza: "Study' (tafiti) zilizofanyika hadi sasa ni chache na 'sample' (sampuri) za wagonjwa wa HIV wamekuwa ni wachache, majibu yaliyopatikana hayapo."

"Mwenye ugonjwa wa kisukari yeye anapata, kwa sababu kinga zake zipo chini na hakuna dawa za kupandisha kinga zake kama ilivyo kwa mgongwa wa UKIMWI. ARV sio kwamba zinakwenda kusaidia kuua virusi vya Corona

"Mgonjwa anayeishi na virusi vya UKIMWI kama hatatumia vizuri dawa za ARV, kinga zake zitakuwa zipo chini kwa hiyo atakuwa kwenye 'risk' (hatari) kubwa ya kupata corona sawa sawa na mwenye ugonjwa wa kisukari," anasema.

Anasema mwenye VVU anaweza kinga zake zikawa zimeshuka na kupata UVIKO-19, na kwamba unawapata wengi wenye kisukari, kwa sababu kinaharibu kinga.

Pia, anagusa kuwa inawapata wazee, kwa sababu kinga zao zimepungua, pamoja na wenye magonjwa kama saratani na presha.

Takwimu za UVIKO-19 duniani hadi Oktoba 12, mwaka huu, jumla ya watu 239,110,636 wameugua, vifo 4,874,702 na waliopona ni 216,365,898.

# Namna ugumu kuvaa barakoa ndani ya madarasa kila aina

Inatoka Uk. 12

tika barakoa hizo ni uwezo kupima namna zinavyokinga bakteria, inapitisha hewa na usafi wake, ikiwa kiwango cha vimelea vya bakteria visivyozidi 30.

Meneja wa Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa TMDA, Gaudencia Simwanza, anasisitiza wamekuwa wakichukua barakoa zinazozalishwa kutoka wauzaji na kuzipima, ili kubaini ubora wake, hata kuzikubali ni salama

Pia, wanapokea bidhaa barakoa kutoka nje ya nchi ambazo asilimia kubwa zimekidhi ubora kuanzia asilimia 70, ambao unakubalika huku wakifanya ukaguzi wakila mara kuangalia ubora wake.

**MWONGOZO WA WIZARA**

Tangu kuingia UVIKO-19 Machi, mwaka jana, serikali imeshatoa miongozo 15, ikiainisha tahadhari za kuchukua kujikinga na maambukizi yake, ikiwamo uvaaji barakoa.

Juni 16, mwaka huu, serikali kupitia waziri anayehusika na afya, Dk. Dorothy Gwajima, anatoa mwongozo kwa jamii kuhusu uvaaji barakoa kwenye maeneo yote ya mikusanyiko, ikiwamo zilizoshonwa na watengenezaji nchini.

Mwongozo unaelekeza wananchi kubeba barakoa wanapotoka nyumbani kukidhi mahitaji, hata kwa waliopata chanjo kamili, huku kukiwapo maelekezo ya watu kuvaa penye huduma za afya, penye mjumuiko wa muda mrefu na usafiri wa umma.

**RAIS SAMIA AWEKA SAWA**

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari katika kuhimiza uvaaji barakoa akijilinda, pia kuwa mfanowa taifa kuingia hatua za kuzuia maambukizi.

Mei 7, mwaka huu, Rais Samia alipokutana na Wazee Mkoani Dar es Salaam, aliwahimiza uvaaji barakoa, kwa sababu ni kundi lililoko hatarini kufikiwa.

Katika shughuli zake kitaifa, Rais Samia anaonekana kwenye barakoa akitimiza kwa matendo kujikinga, pia hamasa kwa umma nchini kufuata mkondo.

Hadi Oktoba 5, mwaka huu, kuna watu 681,736 waliokwishapatiwa chanjo ya UVIKO-19. Hadi juzi Jumatatu, Waziri Afya Dk. Dorothy Gwajima, ametamka zimebakichanjo nane pekee zilizotarajiwa kumalizika wakati wowote.

**KIMATAIFA KULIVYO?**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Tedros Ghebreyesus, anazungumzia mwongozo wa uvaaji barakoa, kwamba penye maambukizi uvaaji barakoa za kitabibu ni lazima, hasa misisitizo kwa watu wazima wenye maradhi mengine au walio katika mazingira hatarishi.


"Kwa kuzingatia ushahidi ambao unazidi kujitokeza, WHO inashauri serikali zihamasishe wananchi wake kuvaa barakoa pale ambako kiwango cha maambukizi ni kikubwa,"anasema.

Kimataifa sasa kunasisitizwa uvaaji barakoa katika sekta ya uchukuzi, hali inayoonyesha hatari ya kusambaa aina mpya ya kirusi Delta, kinachosambaa haraka, hasa kwa wasiochanjwa.

AFYA

# Zifahamu sababu kuu, pia nchi watu wanakoishi miaka mingi

## • Mlo bora, msuguano haupo
## • Kinamama uhai wao unazidi



Moja ya maeneo ya burudani nchini Hispania, kunakotumika kwa mapumziko. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Christina Mwakangale**

KATIKA imani tofauti kidini na kijamii, kuishi muda mrefu ni kudra za Mungu, huku wanasayansi wakijibu mlo unachangia pakubwa, wakieleza kufuata kanuni ni jambo muhimu.

Jeanne Calment kutoka Ufaransa ni binadamu aliyewahi kuishi miaka mingi, akifikisha umri wa miaka 122 na siku 164, kwa mujibu wa rekodi za Guinness.

Mwishoni mwa mwezi uliopita, utafiti unaonyesha nchi tano, zikiwamo Korea Kusini, Japan, Singapore, Uswisi, Hispania na Utalia, watu wake wanaishi miaka zaidi ya 80.

Hata hivyo, gazeti la Nipashe mwaka 2017 iliripoti kuwapo mzee wa umri miaka 127, huku likirejea Italia kukiwapo raia mwenye umri miaka 145.

Watafiti wanaeleza sababu kabla ya kulala, kuna mchango mkubwa kuamua urefu wa umri wa mtu kuishi.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema wastani wa umri kuishi duniani ni miaka 72 mwanaume miaka 69 na miezi nane na mwanamke miaka 74 na miezi miwili.

Kihistoria, binadamu hajawahi kupenda kufa na kutokana na hilo, amekuwa akitafuta mbinu aendelee kubaki kijana.

Hadithi za maji ya chemchem yanachelewesha kifo, hazijawahi kuthibitishwa, lakini kuna nchi wanadumu miaka mingi kwa hilo, kukitajwa zaidi ya wastani miaka 71, kuzidi kuzidi kwingineko duniani.

Ripoti ya Siku ya Furaha Duniani iliyoandaliwa na Umoja wa Mataifa (UN), iliyowasilshwa kuhusu maisha marefu ya nchi tano zilizoko juu kuanzia mwaka 2017.

**WAJAPANI WANAVYOISHI**

Wajapani wanaishi wastani wa miaka 83 na imo katika nchi zenye matarajio ya juu ya maisha marefu ya watu wake, huku Okinawa kilichobatizwa jina 'kisiwa cha wasiokufa' utafiti unaonyesha kuwapo watu zaidi ya 400 wakiwamo wa umri unaozidi miaka 100.

Sababu ni wenyeji wanavyotumia mlo wa tofauti kwa wingi, viazi vitamu na samaki kidogo na kunatajwa mazungumzo baina wazee una uhusiano na umri wao, ikichangia raha zinazomaliza msongo wa mawazo na ubora wa maisha nchini Japan, unatajwa kuwa juu na sababu kuu ni mawazo butu ya wenyeji.

**'MARAHA' YA UHISPANIA**

Mlo wao unatajwa kujaa mafuta ya mizeituni yanayoboresha afya ya moyo, mboga na mvinyo, ikitajwa inawapa uhai zaidi hata kuwaewezesha kuishi umri mrefu wastani wa miaka 82 na miezi nane.

> **Utamaduni unatajwa kuchangia mazingira ya kuwapo maisha marefu ya wakazi. Shuhuda, Bino Chua, anaeleza:"Utaona jinsi watu wengi wanavyokwenda katika klabu za kujenga mwili na kufanya mazoezi katika bustani, ambao kuna watu wanaofanya mazoezi,".**

Miji ya Hispania imeundwa kwa kuzingatia utembeaji kwa miguu zaidi ya magari, huku mkazi Marina Manasyan, akitaja matokeo yake kunakuwapo hewa safi oksijeni, huku hewa chafu ni kidogo.

"Nilipohama kutoka Moscow (Russia) kuja Barcelona, niligundua mara moja kuwa watu hapa wanapenda kutembea au kuendesha baiskeli- au kutembea umbali fulani kwanza, ndio watumie usafiri wa umma, sio kutumia gari."

**AMANI YA SINGAPORE**

Mfumo wa afya wa Singapore unatajwa ni bora zaidi na unawawezesha wakazi kupata huduma za afya, hali inayowawesesha kuishi wastani wa miaka 83 na mwezi mmoja.

Ni nchi inayoongoza duniani kwa rekodi ya chini duniani ya vifo vya wanawake wanapojifungua, wakijikita katika hatua za kuzuia magonjwa, badala ya kutibu.

Utamaduni unatajwa kuchangia mazingira yakuwapo maisha marefu ya wakazi. Shuhuda, Bino Chua, anaeleza:"Utaona jinsi watu wengi wanavyokwenda katika klabu za kujenga mwili na kufanya mazoezi katika bustani, ambao kuna watu wanaofanya mazoezi,".

Bustani ya mazoezi ya wakongwe zaidi wa Singapore inayoitwa 'First Seniors Therapy Park' inatajwa kupunguza msongo wa mawazo na kuwaboreshea wazee afya ya akili, huku kukielezwa Singapore ni vigumu kuzoea tabia mbaya.

**WANAUME WA USWISI**

Nchini Uswisi, wanaume wanaishi miaka mingi kuliko nchi nyingine zote duniani, kukiwapo wastani wa miaka 81 ya kuishi, ikiwa ni moja ya nchi tajiri zaidi duniani inayotoa hakikisho kwa wakazi wake huduma bora zaidi kiafya, kiwango cha juu cha usalama binafsi na maisha bora.

Baadhi ya tafiti zinaonyesha kuwa, maisha marefu nchini Uswiss yanaweza kuhusishwa na ulaji mkubwa wa jibini na milo mingine itokanayo na maziwa.

Ingawa raia wa Uswisi ni wachapakazi, wapenda hali na michezo. Wikendi ni kawaida wakazi wake kwenda kutembea kwingineko Ulaya kwa muda mfupi, penye hali ya hewa safi. Maeneo binafsi, panasifiwa penye shule binafsi ziko bora zaidi kuliko zingine duniani.

**KOREA KUSINI MIAKA 90**

Korea Kusini, inaweza kuwa nchi ya kwanza duniani kufikia wastani wa umri miaka 90 ya matarajio ya kuishi watu wake.

Utafiti wa karibuni unataka vyanzo ni uchumi imara na unaokua, upatikanaji huduma za afya na viwango vya chini vya shinikizo la damu, ikilinganishwa na nchi nyingine duniani

Mlo wa Wakorea kawaida umejaa vilivyochachishwa, vinaaminiwa kushusha viwango vya mafuta mwilini na kuongeza kinga shidi ya maradhi saratani.

Ni chakula kinachotajwa kuwa na wanga mwingi utokanao na mimea na kina virutubisho vingi.

Wanatajwa kuwa na uhusiano binafsi na wa umma, inayowawezesha Wakorea kuimarisha viwango vya juu vya maisha bora, wakichangamana kuwaondolea msongo wa mawazo.

**NAFASI YA MLO**

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema wastani wa umri wa kuishi binadamu duniani ni miaka 72, mwanamume miaka 69 na miezi nane, huku mwanamke yake miaka 74 na miezi miwili.

Kiafya kuna usemi 'mlo kabla ya muda wa kulala ni tiketi ya safari yako kuelekea umri, lakini kituo kipi utashuka na kwa umbali gani utashukia, iwe kilomita fupi au ndefu, inatokana na lishe,

Inalaezwa, ili mtu aishi umri mrefu, anahitajika kunywaji divai au mvinyo nyekundu, chai ya kijani na sukari 'kiduchu' au kutokula kabisa wakati wa kulala na kula mkate wa nafaka (ngano) tupu.

Wanasayansi wanasema chai ya kijani (green tea) ina kitu kiitwacho 'antioxidants', ambacho ni muhimu katika kulinda seli za mwili dhidi ya magonjwa ya moyo na saratani na inafanya kazi vizuri zaidi mwilini kuliko chai ya kawaida au kahawa.

Pia, unywaji wa divai nyekundu baada ya saa 11.00 jioni inatajwa ni kitu kinachomsaidia mtu aishi miaka mingi. Manazuoni Dan Buettner, ana hoja ya kitafiti kwamba matumizi ya pombe kiasi una manufaa kiafya.

Pia, ushauri wa kisayansi kwenye lishe, ulaji wa mkate uliotengenezwa na nafaka tupu; kula mapema kidogo au kutokula kabisa usiku wakati wa kulala, kunasaidia kujenga afya na kuutuliza mwili kupumzika kwa viwango vinavyokubalika.

Daktari Kristen Willeumier anasema, umri mrefu unaanzia pale mwili usipokumbana na matatizo, hivyo muda mrefu wa mapumziko.

**• Makala hii kwa msaada wa taarifa za mtandao.**





## DC awaonyesha fursa kiuchumi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mwanahamisi Munkunda, amewataka wakazi wa mkoa wa Dodoma kuwekeza kwenye kilimo cha zao la zabibu na alizeti ili kujikwamua kiuchumi.

Munkunda, alitoa wito huo jijini hapa wakati wa uzinduzi wa wiki ya mavuno chini ya kampeni ya anza na hekari moja yanayoratibiwa na kampuni ya (JATU PLC).

Alisema indapo wananchi watawekeza katika kilimo ni wazi kuwa wataondokana na umaskini wa kipato na kuachana na kilimo cha kimazoea.

Aidha, alisema wakulima hivi sasa wanatakiwa kubadilika kwa kulima kilimo cha kisasa na chenye tija hasa zao la zabibu na alizeti kwa mkoa wa Dodoma ambapo linaonekana kuwa na tija.

Alisema mazao hayo mawili kwa mkoa wa Dodoma hivi sasa ndiyo yamekuwa na tija kwa wakulima hivyo hawana budi kuwekeza nguvu zao ili kuondokana na umaskini.

Katika kuhamasisha kilimo alisema mkoa wa Dodoma umetenga zaidi ya hekari 800,000 ili kuhamasisha kilimo cha zabibu na ufuta.

"Mkoa kwa kushirikiana na serikali umekuwa na ukifanya jitihada mbalimbali za kuboresha mazingira ya kilimo ikiwemo kutenga maeneo kwa ajili ya kilimo hivyo wananchi hawana budi kuchangamkia fursa zilizopo kwenye kilimo," alisema.

Naye Meneja wa kampuni ya JATU PLC, Mohamed Simbano, alisema kampuni hiyo kazi yake kubwa ni kutoa hamasa kwa jamii hususani vijana ili kuwekeza zaidi katika kilimo.

Alisema kwa sasa JATU imekuwa ikitoa elimu ya kilimo hasa katika maeneo mbalimbali kwa kuishawishi jamii kuwekeza katika kilimo.

Katika hatua nyingine meneja huyo alisema hadi sasa wamefanikiwa kulima heka, 20,312 za mazao ya chakula na mafuta katika baadhi ya maeneo.

Kadhalika, alisema kampuni hiyo inaendelea kutoa hamasa ya kukuza na kuboresha kilimo kwa lengo la kuondokana na umasikini wa kipato.

# RC Mtaka azipa wilaya jukumu chanjo Uviko-19

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameziagiza kamati za afya za wilaya kuweka mikakati ya kufikisha elimu ya chanjo ya UVIKO-19 katika maeneo yote ili kuiwezesha jamii kutambua manufaa ya kuchanja.

Mtaka alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati wa kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi cha Mkoa kufanya tathmini juu ya mpango jamii shirikishi na harakishi wa chanjo ya UVIKO-19.

"Hakikisheni kuwa huduma hizo zinawafikia wananchi katika maeneo yote yenye mikusanyiko kama sehemu za ibada misikitini, makanisani, kwenye makongamano sambamba na sehemu za vituo vya mabasi," alisema Mtaka.

Aidha, Mtaka alisema Ofisi ya Mkoa tayari wameshapokea shehena mpya ya chanjo ya Sinopharm dozi 50,390.

"Sasa hizi kamati ziende huko sehemu ambapo watu wapo mkatoe elimu juu ya chanjo hii mpya baada ya ile nyingine kuisha mkawape elimu na wataalamu pia mkatoe elimu juu ya chanjo hii," alisema.

Mratibu wa chanjo mkoa wa Dodoma, Francis Bujiku, alisema Mkoa wa Dodoma awali ulipokea jumla ya dozi 50,000 za chanjo ya Uviko -19 ya JJ na Agosti 3, 2021 ulizindua kampeni ya uchanjaji na hadi kufikia Oktoba 5, mkoa ulikuwa umemaliza chanjo zote zilizopangwa kwa asilimia 100.

"Baada ya kuona tumemaliza zile zilizopangwa tukaomba chanjo za ziada 6,515 kutoka mikoa ya Geita chanjo 5,000, Iringa1,515 na hadi kufikia Oktoba 13 jumla ya wananchi 52,599 walichanja chanjo ya UVIKO-19," alisema Bujiku.

Kadhalika alisema kutokana na uanzishwaji wa chanjo ya Uviko-19 katika Mkoa wa Dodoma, Agosti 3, 2021wananchi wamepata elimu na vituo vikuwa 28 vya kutoa chanjo na kuongezeka hadi kufikia 381, ambapo walengwa 52,629 wamepatiwa chanjo hadi kufikia Oktoba 14, 2021 sawa na asilimia 93 ya lengo la kuchanja walengwa 56,515.

Kuhusu uanzishwaji wa chanjo mpya, Bujiku alisema serikali imejipanga kuwa na utaratibu wa utekelezaji wa uanzishwaji wa chanjo hiyo mpya ya Sinopharm ambao utaleta matokeo makubwa.

Hata hivyo, alisema vituo 381 vitaendelea kutumika kutoa chanjo hiyo pamoja na huduma ya mkoba katika maeneo yote ambapo chanjo hiyo itatolewa mara mbili dozi hiyo ya pili itatolewa siku 28 baada ya chanjo ya kwanza huku akiwasisitiza wananchi kutopuuzia kurudi kumalizia dozi hiyo ya pili.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumza wakati wa kikao kazi cha wafanyakazi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wengi wasumbuliwa na macho mkoani Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASILIMIA 75 hadi 85 ya wakazi wa mkoa wa Dodoma wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ya macho ikiwamo uoni hafifu pamoja na ugonjwa wa trakoma.

Hayo yalibainishwa na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho kutoka katika Hospitali ya Rufani ya mkoa wa Dodoma, Dk. Msigalo Erasto, wakati akielezea hali ya magonjwa mbalimbali ya macho katika maadhimisho ya wiki ya afya ya macho duniani.

Dk. Erasto alisema moja ya chanzo cha tatizo la uoni hafifu ni matumizi ya simu kwa muda mrefu hususani mwanga wa simu za mkononi, kuangalia runinga (televisheni) na kompyuta kwa muda mrefu.

Alisema watu wengi wanatatizo la afya ya macho kutokana na mwamko mdogo wa kupima afya ya macho mara kwa mara.

Akizungumzia kuhusu Mkoa wa Dodoma, Dk. Erasto alisema wagonjwa wengi wamekuwa wakihusisha matatizo ya macho na imani za kishirikina.

"Tumeona kuwa mkoa wa Dodoma una wagonjwa wengi wa macho na kibaya zaidi wamekuwa wakihusisha ugonjwa wa macho na imani za kishirikina.

"Tunapenda kuhimiza jamii kujitokeza na kujenga desturi ya kupima afya ya macho ili kuhakikisha wanapata matibabu kwa wakati pale wanapogundulika kuwa na matatizo," alisema.

Aidha alisema katika wiki ya maadhimisho ya afya ya macho duniani wanafanya upimaji wa huduma ya macho bure hivyo wanahamasisha jamii kuona umuhimu wa upimaji macho na linapotokea tatizo wapatiwe matibabu stahiki.

Aidha, mmoja wa wakazi wa Jiji la Dodoma, Ashura Mohamed, alisema wanaiomba serikali kusogeza huduma za afya ya macho jirani na wananchi.

"Elimu ya upimaji wa afya ya macho bado haijaeleweka kwa watu wengi lakini pia huduma zinapatikana kwa tabu, tunachoomba ni serikali kusogeza huduma hiyo karibu na jamii," alisema.



# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mkewe, kunyofoa viungo vyake

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mbeya, imemhukumu kunyongwa hadi kufa Mateso Shantiwa, mkazi wa Kitusi wilayani Mbeya, baada ya kupatikana na hatia ya kumuua mke wake Zaina Mela na kunyofoa viungo mbalimbali ili apate utajiri.

Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, mwenye mamlaka ya nyongeza kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya kusikiliza mashauri ya mauaji, ndiye alitoa hukumu hiyo jana.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Laizer alisema amemhukumu mtuhumiwa kwenye shtaka hilo namba 18/2017 baada ya kuridhishwa na ushahidi wa upande wa Jamhuri bila kuacha shaka yoyote kuwa mshtakiwa alimuua mkewe.

Hakimu Laizer alisema mshtakiwa Shantiwa alikuwa akituhumiwa pamoja na wenzake wawili ambao hawakukamatwa ambao alishirikiana nao kumuua mke wake na kunyofoa viungo kadhaa vikiwamo masikio na matiti kisha kupelekwa kwa mganga aliyewaahidi kupitia vitu hivyo angewatengenezea utajiri wa kudumu.

Kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa wakati wa usikilizwaji shauri hilo, mshtakiwa Shantiwa alishirikiana na wenzake wawili kutekeleza mauaji ya mkewe kwa kuondoa viungo ambavyo ni matiti yote mawili, macho, vipande vya masikio na sura ya marehemu ili kwenda kutengenezewa utajiri.

Hakimu Laizer alisema alizingatia maelekezo ya pande zote mbili na maoni ya wazee washauri wa mahakama, lakini zaidi, mahakama imeridhika mshtakiwa kuhusika moja kwa moja kumuua mke wake na watu alioshirikiana nao kwa tamaa ya kupata utajiri licha ya kwamba mshtakiwa alikuwa akikana kutenda kosa hilo.

Mshtakiwa alikuwa akiwakilishwa na Wakili Hilda Mbele na kabla ya hukumu, aliomba kupunguziwa adhabu lakini upande wa Jamhuri kupitia wakili aliyekuwapo mahakamani, Davice Msanga, ukaiomba mahakama kutoa adhabu stahiki ili iwe fundisho kwa wengine ambao wanakubali kudanganywa na waganga wa kienyeji.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa Shantiwa (34), alidaiwa kutenda kosa hilo Aprili 22, 2017 akishirikiana na wenzake wawili, jambo ambalo ni kinyume cha kifungu namba 196 na 197 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2002.




Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Asajile John (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa mbunifu wa mashine ya kuvunia mazao jamii ya kunde kutoka Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Joshua Joasi (kulia ), wakati wa maonyesho ya Wiki ya Ubunifu, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# 'Unywaji kahawa bado uko chini'

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASILIMIA saba ya Watanzania ndio wanakunywa kahawa nchini huku asilimia 93 ya kahawa inayozalishwa nchini inasafirishwa kwenda nje ya nchi.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Ubora wa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), Florian Ndunguru, alisema mpango walio nao bodi ni kuhakikisha hadi kufikia mwaka 2025 unywaji wa kahawa unafikia asilimia 15 hadi 20.

Aliongeza kuwa ubora wa kahawa inayozalishwa nchini umeonyesha kuongezeka, hatua ambayo itasaidia kukuza kipato cha kaya za wakulima wa zao hilo, licha ya kuwapo kwa unywaji mdogo wa kahawa.

Nduguru alisema kwa msimu wa mwaka huu, ubora wa kahawa umeimarika ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita.

"Kahawa ni kinywaji kinachotumiwa na watu wengi duniani. Kuimarika kwa ubora wa zao hilo ni matokeo ya jitihada za wakulima zinazotokana na kuzingatia mbinu bora za uzalishaji na utumiaji wa teknolojia za kilimo zinazolenga kuongeza tija ya uzalishaji, ingawa unywaji wa kahawa kwa hapa nchini bado ni mdogo," alisema.

Naye Meneja wa TCB, Sijali Bowa, alisema vyama vya ushirika vinavyosimamia wakulima vina nafasi ya kununua zao hilo na kuendelea kulisindika.

Alisema kupitia vyama vya ushirika, wakulima wanaweza kunufaika kwa sababu kampuni nyingi zitakuja kununua kwa bei nzuri kwa sababu ya ubora na usindikaji uliofanywa.

Baadhi ya wadau wanaochangia kwenye mnyororo wa thamani wa kahawa walisema bado kuna tatizo katika kuzalisha kahawa bora.

Miongoni mwa wadau hao, Samora Mnyaonga, kutoka Shirika la Café Afrika alisema inahitajika nguvu ya pamoja ili kumsaidia mkulima kuzalisha kwa tija ikiwamo kuongeza ubora ili kumudu soko la ushindani kimataifa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema serikali inathamini kahawa kama zao kuu la biashara na inaendelea kuweka mikakati ya kuendeleza zao hilo kuanzia hatua ya upatikanaji wa mbegu bora mpaka sokoni.

Kahawa ni moja kati ya bidhaa zinazoshika nafasi ya pili katika mazao ya biashara ikitanguliwa na mafuta ya kula, takribani vikombe milioni 2.3 vya kahawa hunyewa kila siku duniani na Oktoba Mosi kila mwaka ni Siku ya Kahawa Duniani.

## Ujenzi kituo afya wanukia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya Sh. milioni 524 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ilemi ili kuwaondolea adha wakazi wa eneo hilo kutumia muda na gharama kufuata huduma katika maeneo mengine.

Kata ya Ilemi haijawahi kuwa na kituo cha afya tangu kupatikana kwa uhuru wa nchi, hivyo kukamilika kwa ujenzi huo, kutawasaidia wananchi kupata huduma za matibabu kwa wakati.

Akizungumza na Nipashe jana, Meya wa Jiji la Mbeya, Door Issa Mohamed, alisema katika kufanikisha ujenzi huo, Halmashauri ya Jiji la Mbeya imetenga Sh. milioni 200 kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mohamed alisema kituo hicho kinatarajiwa kujengwa kwa gharama ya Sh. milioni 524.6 kwa awamu ya kwanza na kwamba fedha zitaendelea kutolewa kadri zitakavyokuwa zinapatikana kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

"Tutakijenga kituo hiki kwa kutumia utaratibu wa 'Force Account', hivyo nawaomba wananchi mjitokeze kujitolea kufanya kazi hapa maana utaratibu huu unataka sana ushiriki wa wananchi kwenye utekelezaji," alisema Mohamed.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, Amede Ng'wanidako, aliwataka wananchi kuendelea kulipa kodi na tozo mbalimbali za serikali ili fedha za kutekeleza mradi huo pamoja na miradi mingine zipatikane.

Alisema ili kufanikisha miradi kila Mtanzania anatakiwa kuchangia kwa kulipa ushuru na kodi ili kuepuka kutegemea misaada kutoka nje ambayo kwa kiwango kikubwa huwa na masharti magumu.

**"Tutakijenga kituo hiki kwa kutumia utaratibu wa 'Force Account', hivyo nawaomba wananchi mjitokeze kujitolea kufanya kazi hapa maana utaratibu huu unataka sana ushiriki wa wananchi kwenye utekelezaji," alisema Mohamed.**



## Serikali yasaka fedha ujenzi wa hospitali ya kisasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema nia ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya kisasa ya Binguni Wilaya ya kati Unguja ipo na kazi kubwa inayofanyika sasa ni kutafuta fedha kutoka kwa washiriki wa maendeleo.

Waziri wa Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, aliyasema hayo jana alipozungumza na mfanyabiashara kutoka Dubai, Ahmada Al-Falasi, baada ya kutembelea eneo la kiwanja ambacho mfanyabiashara huyo ametia nia ya kujenga hospitali ya kisasa huko Fumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Mazrui alisema mradi wa hospitali ya kisasa ya Binguni haujatelekezwa, na serikali imeona ni bora kutafuta wafadhili watakaogharamia ujenzi huo ambao ni mkubwa ukiwa na huduma za chuo cha kufundishia wanafunzi.

Alisema Zanzibar inahitaji hospitali ya kisasa yenye uwezo wa kutibu maradhi mbalimbali ikiwamo yasiyoambukiza ambayo yanaongoza kwa kusababisha vifo.

Alisema wanamkaribisha mfanyabiashara Al-Falasi kujenga hospitali ya aina hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa itapunguza mzigo wa serikali kuwasafirisha wagonjwa kwenda nje ya nchi.

"Zanzibar inahitaji huduma za afya bora ambazo zitasaidia kukabiliana na changamoto ya maradhi tishio yanayosababisha vifo kwa wananchi wengi nchini," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Sharifu Ali Sharifu, alisema wapo katika hatua ya mwisho ya kuchagua eneo ambalo litajengwa hospitali hiyo huko Fumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema eneo la Fumba lipo katika ukanda wa maeneo huru ya uchumi na uwekezaji ambayo yametengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa.

"Tumeanza kulikaguwa eneo la Fumba maeneo huru ya uwekezaji kiuchumi ambalo ni zuri kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya kisasa yenye huduma zote ikiwamo utafiti," alisema.

Mwekezaji Ahmada Al-Falasi alisema nia yake ni kujenga hospitali kubwa yenye uwezo wa kutibu maradhi mbalimbali na kuweza kupata tiba yake hatua ambayo itapunguza kusafirisha wagonjwa kwenda nje ya nchi.

"Nimetembelea maeneo mengi kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya kisasa ambapo nimechagua Zanzibar kutimiza ndoto yangu ya kuwa na hospitali kubwa ya kisasa ya kutoa tiba," alisema.

# Shirika la Ndege Ufaransa kuuimarisha utalii Zanzibar

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

SHIRIKA la Ndege la Ufaransa limeanza safari zake za kupeleka abiria Zanzibar, ndege yake ikiwasili kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ikiwa na abiria 175 juzi.

Mapokezi ya ndege hiyo aina ya Boeing 787-9 yalifanyika chini ya mapokezi ya mawaziri watano wa Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiongozwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasili kwa ndege hiyo kiwanjani hapo, Waziri Mbarawa alisema shirika hilo miaka ya nyuma lilikuwa linafanya safari zake Zanzibar lakini likasitisha na kwa sasa historia mpya imeandikwa na hivyo kuonyesha kuwa wadau wa maendeleo wana imani Serikali ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema serikali zote mbili zitaendelea kujipanga kuhakikisha zinawekeza katika miundombinu mizuri na ya kisasa ili kuyafanya mashirika ya ndege mengi kufika Tanzania ikiwamo Zanzibar.

Alisema ujio wa ndege hiyo ni fursa kubwa, hivyo kuwataka wale wote watakaopata fursa ya kuhudumia shirika hilo na mashirika mengine, kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa ili watalii wengi kufika na kuchangia uchumi wa nchi.

Waziri wa Biashara za Nje na Uchumi wa Ufaransa, Franck Reister, alisema usalama wa abiria ni jambo muhimu kuhakikisha kwa muda wote wanapokuwa nchini wanakuwa salama huku wakifanya shughuli zao kwa utulivu.

Alisema Zanzibar inayo nafasi kubwa ya kupiga hatua katika maendeleo ya sekta ya utalii kutokana na kuwa na vivutio mbalimbali vinavyotoa nafasi kwa wageni hao kuja mara kwa mara nchini.

"Shirika la Ndege la Ufaransa limerudisha tena huduma za usafiri kwa abiria katika kisiwa cha Zanzibar baada ya kuridhishwa na mazingira ya utulivu na usalama wa wageni wake," alisema.

Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Omar Siad Shabani, alisema ujio wa ndege hiyo utaleta wageni kwa ajili ya utalii, uwekezaji na biashara huku akilipongeza shirika hilo kwa kuamua kurejesha safari zake Zanzibar.

Alisema serikali itawahakikishia kila aina ya msaada wanaohitaji katika kuhakikisha uwapo wao unakuwa mzuri na wa kibiashara kwa pande zote mbili.

"Matumaini yangu kwamba siku zijazo kampuni hizi pia zitafikiria kuanza kuleta ndege za mizigo ili kuifufua Zanzibar kibiashara hasa ikizingatiwa kuwa wafanyabiashara wengi wanalalamika upatikanaji wa safari za ndege, hivyo ujio wa ndege hizo itaifungua Zanzibar kibiashara," alisema.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Muhamed Mussa, alisema ndege hiyo itafanya safari zake Zanzibar siku mbili kwa wiki ambapo kwa safari moja itakua na abiria 175, akiitaja ni hatua kubwa kwa Zanzibar.

Alisema uwapo wa ndege hiyo itakuwa ni fursa kubwa sana Zanzibar kurudi katika soko la utalii ambalo ni sekta mama inayochangia pato la taifa.

Alisema Serikali ya Zanzibar itaendelea kuchukua tahadhari ya corona ili kuwaweka salama wageni wote wanaofika nchini na kuchukua hatua za kiusalama.




Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Lela Mohamed Mussa (katikati) na Waziri wa Biashara za Nje na Uwekezaji wa Ufaransa, Franck Riester (kulia), wakikata utepe kuashiria uzinduzi wa safari ya ndege ya kitalii kutoka Ufaransa hadi visiwa vya Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri ataka ubunifu chuo utafiti wa kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Umwagiliaji amewataka wataalamu wa Chuo cha Kilimo na Utafiti cha Kizimani Zanzibar kuongeza ujuzi na ubunifu wa mbegu za mazao ya mizizi ikiwamo muhogo ili kuongeza uzalishaji kwa wakulima.

Dk. Soud Nahoda, alitoa rai hiyo jana alipozungumza na wataalamu wa chuo hicho huko Kizimbani, Unguja.

Alisema malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujitosheleza kwa chakula kwa kuongeza uzalishaji kwa wakulima ili nao wawe na kipato kikubwa zaidi.

Alisema wataalamu wa kilimo wanakabiliwa na jukumu hilo na kuongeza utaalamu utakaosaidia na hatimaye kuwawezesha wazalishaji wa kilimo kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

"Wizara ya Kilimo tumepewa jukumu la kuhakikisha tunaongeza uzalishaji kwa kujitosheleza kwa chakula hatua ambayo italeta tija kwa wakulima wetu," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mariamu Abdalla Sadalla, alisema uzalishaji wa mazao ya mizizi umeongezeka katika mwaka 2020 na kufikia tani 158,465 za muhogo.

Alisema uzalishaji wa ndizi pia umeongezeka na kufikia tani 65,321 hatua ambayo imeongeza kipato kwa wakulima wa mazao hayo sambamba na uzalishaji wa mazao mengine ikiwamo magimbi na viazi vitamu.

Aliyataja mafanikio hayo ni matokeo ya Kituo cha Kilimo cha Kizimbani kufanya kazi ya ziada ya ubunifu wa kitaalamu wa uzalishaji wa mbegu zenye uwezo mkubwa wa uzalishaji wa mazao.

"Kituo cha uzalishaji wa mbegu cha Kizimbani kimepata mafanikio makubwa ya uzalishaji wa mbegu za mazao ya mizizi kwa wakulima na kuleta uzalishaji mkubwa kwa wakulima na kupata kipato," alisema.

Mtaalamu wa uzalishaji wa mbegu katika Chuo cha Utafiti wa Kilimo Kizimbani, Fatuma Mohamed, alisema wakulima wengi wameitikia wito na kuchukuwa mbegu zinazozalishwa katika kituo hicho ambapo katika kipindi cha miaka miwili ya majaribio mafanikio makubwa yamepatikana.

"Majaribio ya mbegu tunazozalisha yameleta matumaini makubwa kwa wakulima kupata kipato kikubwa huku aina ya mbegu sita za muhogo kuonyesha mafanikio ikiwamo utamu," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHABANI DAUDI** anatangaza kupotelewa na chati cha **UALIMU daraja III A** chenye index namba **E 522/027** kilichotolewa na **CHUO CHA UALIMU KINAMPANDA** mwaka **1993** ,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MUL/RB/4448/2013**

## KUPOTEA KWA CHETI



**STEPHANO MAPENZI ELIEJENJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1363-0131** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TEMBONI SEKONDARI mwaka 2018.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Control No: **991083062877.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ESTELINA EMMANUEL MLAMBIA** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha nne yenye index namba **S4176/0001** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **IMAULUMA mwaka 2020**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/GOG/RB/483770/2021**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**AISHA SULEIMAN KITUNGULU** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S3795/0002** iliyotolewa na **YEMENI SEKONDARI mwaka 2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MBU/RB/500124/2021.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



116522002

**ELIA MARWA NYAMHANGA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S0132/0580** iliyotolewa na MILAMBO HIGH SCHOOL mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/502736/2021.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.315/2021**

Ombi la **EDDA ASIMWE LUTTA & KELVIN ALPHONCE MAGUMBILA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ALFRED KAHANJU CHITIKI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 22/11/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukagulia.
**Tarehe 20/10/2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.312/2021**

Ombi la **MUHIDINI SEIF SELEMAN** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu
**IDD SEIF SELEMANI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 03/11/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukagulia. **Tarehe 13/10/2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo mjini morogoro**
**Usimamizi wa mirathi 314/2021**

Ombi la **HAMISI AHMADY MADOWEKA**
Msimamizi wa mirathi ya marehemu
**SALIM SELEMAN MADOWEKA**

Kwa watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 23/11/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo kuwa msimamizi wa mirathi hiyo Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA RUFAA JINAI Na. 77 /2019**
**(Asilia Shauri la Hujuma Na.1/2018,**
**Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**
**JAMHURI.........................................................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE.....MJIBU RUFAA NA.1**
**MATHEW ELIKANA MWANJALA...MJIBU RUFAA NA.2**
**SHABAN MKWICHE.........................MJIBU RUFAA NA.3**
**KWA BWANA:1. KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE**
**2. MATHEW ELIKANA MWANJALA**
**3. SHABAN MKWICHE**

**POPOTE ULIPOTANZANIA.**

Mnaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe 25/10/2021 siku ya Jumatatu Saa 3.00 asubuhi bila kukosa.
**ELEWENI KWAMBA** mkikosa kufika siku hiyo,Shauri litasikilzwa upande mmoja na Uamuzi kutolewa bila ninyi kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa **Mahakama hii leoTarehe 27/09/2021.**

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

---

**THE REGISTRATION OF DOCUMENT CAP 117 CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

By the deed poll I PAULO BASILI MASSAWE (New name) of Karatu utterly renounce, relinguish and abandon the use of my former names of PAULO BASILI DIYAMI(Old Name) in lieu of and substitution of my former name PAULO BASILI MASSAWE (New name).

The name of PAULO BASILI DIYAMI has been used in NIDA (This is the reason for changing the name).

For the purpose of evidencing such determination, I hereby declare that I shall at all times have after in all records, deeds documents other writings and in all actions, suit and proceedings as well in public and private dealings and transactions and on all accasion whatsoever use and subscribe the said the name PAULO BASILI MASSAWE (New name) so relinguish as aforesaid the name PAULO BASILI DIYAMI (Old Names).

I hereby expressly authorize and require all and ever person and person whomsoever at all times after the date hereof to designate describe and address me by the adopted name of PAULO BASILI MASSAWE (New name) accordingly.

In witness whereof I have submitted my (Old Names) PAULO BASILI DIYAMI into PAULO BASILI MASSAWE (New name) In witness thereof I have set my hand at Karatu.

**This 5 day of October 2021**
**Signed and delivered by the said**
**PAULO BASILI MASSAWE who is known to me personally**
**This 5th October, 2021.**

---

## HATI YA KIAPO

Mimi **STEVEN GILBERT MACREA** wa Makorora Tanga, Mkristo, mtu mzima naapa na kutamka kupotelewa kwa "Offer" ya kiwanja Na. 201, Kitalu "D" Makorora Jiji la Tanga. Kiapo hiki nimetoa ili niweze kupatiwa nakala ya "Offer" hiyo na Ofisi ya Mipango Miji ya Jiji la Tanga au Polisi.
**IMEAPWA** na **KUTOLEWA** na huyo **STEVEN GILBERT MACREA**
Ninayemfahamu / aliyetambulishwa
Kwangu na...................
ambaye ninamfahamu hii leo tarehe 27 September, 2021.
MBELE YANGU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa wa Njombe**

Usimamizi wa mirathi na 92/2021 katika shauri la mirathi ya LAUTERY MICHAEL MBWILO Marehemu wa katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyotolewa na FELISTER PETER MGIMBA mwombaji.

**TANGAZO KWA UMMA**

***(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za umimamizi wa mirathi mahakama ya mwanzo)***

watu wote wanaodai kuwa na uhusiao wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria tarehe 18 mwezi 11 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza leta mahakamani kukaguliwa.

. Wosia wa merehemu huyo upo mahakamani na unaweza kaguliwa.
. Marehemu hakuacha wosia.
. Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 18 mwezi 10 mwaka 2021**

HAKIMU MKAZI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 141 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE AHMED NGAJENI MULAGWA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY ELIWAJA MLULA TIGHA.....................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of 11,2021.

Dated at Dodoma this 08 day of 10, 2021.

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

116521801

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA.1/2020**

**(Asilia shauri la jinai Na.82/2018, Mahakama ya Wilaya Mtwara)**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA......................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**HAMISI MOHAMED @NAUDENDE......... MJIBU RUFANI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: HAMISI MOHAMED@NAUDENDE**
**NAMNYAMBA**
**MTWARA**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA RUFAA HII MNAMO TAREHE 17/11/2021 SAA 2:30 BILA KUKOSA.

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA LEO HII TAREHE 06/10/2021

A. H. MSUMI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

Attachments area

116521902

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TANZANIA DOMESTIC APPLIANCE MANUFACTURERS LTD**

inatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 420 ADB – NISSAN PATROL.** Chassis namba **JNITC546120500951.** Engine namba **TD42137338.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/501851/2021.**

116521702

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Shambulio laua 13 ndani ya basi

**Damescus, SYRIA**

WATU wasiopungua 13, wengi wao wakiwa wanajeshi, wameuawa na wengine watatu wamejeruhiwa katika shambulio la basi katikati mwa mji wa Damascus.

Mabomu mawili yalilipuka wakati basi lililokuwa limebeba wanajeshi lilipopita chini ya daraja mjini Damascus.

Milipuko hiyo ilisikika sehemu kubwa ya mji mkuu wa Syria na kutikisa baadhi ya maeneo ya mji huo.

Kifaa cha tatu cha kulipuka kiligunduliwa na kuteguliwa na wataalam wa kijeshi, kulingana na Shirika la Habari la Serikali Syria (SANA).

Mamlaka nchini Syria haijaeleza ikiwa shambulio hilo lilikuwa la kujitoa muhanga au bomu lililofyatuliwa kwa mbali.

Picha zilizorushwa na vyombo vya habari, zinaonyesha basi lililoteketezwa kwa moto milipuko hilo baada ya maofisa wa Zimamoto kuingilia kati.

Tangu wanajeshi wa serikali ya Syria walipopata tena udhibiti wa mji wa Damescus na viunga vyake takriban miaka mitatu iliyopita, hali ya utulivu imetawala na mashambulio kama hayo ni nadra kutokea.

Shambulio la mwisho lilitokea mwaka mmoja uliopita, wakati mufti wa Kisuni wa Mkoa wa Damascus, Adnane al-Afyouni, alipouawa katika mlipuko wa bomu lililotegwa katika gari lake.

Shambulio hilo lilitokea Qoudsaya, kitongoji cha karibu cha Damescus.

Shambulio hilo la jana kwa ni tukio la kipekee na ni uvunjaji wa mfumo wa usalama uliowekwa katika mji mkuu wa Syria na viunga vyake.

RFI

## Misri yaapisha majaji 90 wanawake

**Cairo, MISRI**

MISRI kwa mara ya kwanza, imewateua wanawake 98 kuwa majaji katika moja ya vyombo vikuu vya idara ya mahakama, Baraza la Kuu la Serikali.

Majaji hao waliapishwa mbele ya jaji mkuu wa baraza hilo katika hafla iliyofanyika katika mji mkuu Cairo, juzi.

Ni miezi kadhaa baada ya Rais Abdul Fattah al-Sisi, kuwataka wanawake wajiunge na vyombo vikuu viwili vya mahakama ikiwamo Baraza na Mashtaka ya Umma.

Tangu kuanzishwa mwaka 1946, baraza la serikali limekuwa likiwateua wanachama wa kiume pekee na hadi sasa limekataa kabisa maombi ya wanawake

Katika miaka iliyopita, wanawake walipinga uamuzi wa baraza hilo, wakisema kuwa wanabaguliwa.

**BBC**

# Masharti ya kutotoka usiku yaondolewa Kenya

**Nairobi, KENYA**

RAIS Uhuru Kenyatta ameondoa masharti ya marufuku ya kutotoka nje kuanzia saa nne usiku hadi saa 10 alfajiri nchini.

Akizungumza katika sherehe za kuadhimisha sikukuu ya mashujaa, Kenyatta amesema kwamba hatua hiyo imekuja kutokana na kupungua kwa visa vya maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema kwamba kufikia sasa ni watu milioni tano, waliopata chanjo ya ugonjwa wa corona na kuongeza kuwa serikali yake inaelekea kufikia lengo lake la kuwapatia chanjo hiyo watu milioni 10 ifikapo Desemba, mwaka huu.

Hata hivyo Rais Kenyatta aliwataka Wakenya kuchukua jukumu la kujilinda na kuwalinda wapendwa wao.

Hatua hiyo inajiri wakati Wakenya wakitaka serikali kuondoa masharti hayo kwa lengo la kuendelea na shughuli zao ikiwamo biashara za kawaida.

Uhuru alisema kwamba baraza la viongozi wa kidini, wafanyakazi wa afya na maofisa wa usalama walifanya kazi nzuri katika kuhakikisha kwamba masharti ya kukabiliana na ugonjwa huo yanaheshimiwa.

**BBC**



Barabara iliyofunikwa na kifusi cha udongo kutokana na maporomoko ya ardhi kufuatia mvua zilizonyesha Kaskazini mwa nchi ya India huku Kikosi cha Taifa cha Kukabiliana na Maafa (NDRF) kikiwaokoa wakazi wa kijiji cha Chhara jirani na Nainital, Uttarakhand, jana.
**PICHA: AP**

# 100 wafariki kwa mafuriko, maporomoko ya ardhi

**New Delhi, INDIA**

ZAIDI ya watu 100 wamefariki dunia baada ya siku kadhaa za mafuriko makubwa na maporomoko ya ardhi, yaliyoharibu barabara na nyumba nchini India na Nepal.

Viongozi wamesema jana na kwamba kuongeza watu wengi hawajulikani waliko.

Jana, idadi iliongezeka nchini India hadi watu 85 waliofariki dunia na 11 hawajulikani waliko, huku Nepal idadi ya vifo ikiongezeka hadi 31 na 43 hawajulikani waliko.

Mamlaka ya hali ya hewa nchini India imeongeza muda wa tahadhari wiki hii na kutabiri kwamba, mvua kubwa zitanyesha katika ukanda huo kwa siku mbili zijazo.

Katika eneo la Uttarakhand Kaskazini mwa India, viongozi walisema watu 46 walifariki dunia katika siku za hivi karibuni na 11 hawajulikani waliko.

Katika Jimbo la pwani la Kerala (Kusini), Mkuu wa Serikali katika jimbo hilo, Pinarayi Vijayan, amebaini kwamba idadi ya vifo ni 39.

Karibu wahanga 30 Uttarakhand walipoteza maisha mapema juzi katika visa saba tofauti katika Mkoa wa Nainital ulioathiriwa vibaya baada ya maporomoko ya ardhi na kuharibiwa kwa miundombinu, hali ambayo ilisababishwa na mafuriko makubwa.

Watu watano wa familia moja walifukiwa katika nyumba yao, alisema ofisa wa eneo hilo, Pradeep Jain.

Waathiriwa wengine watano waliuawa katika maporomoko ya ardhi yaliyotokea wilayani Almora, Kaskazini mwa Uttarakhand na nyumba yao kuzama chini ya mawe na matope.

Kwa sababu ya maonyo ya hali ya hewa, mamlaka imeamuru shule zifungwe na kupiga marufuku shughuli zote za kidini ikiwamo za watalii katika jimbo hilo.

**RFI**

HABARI MICHEZO

# SERENGETI LAGER YAJA NA 'NJE YA DIMBA NA STARS'

**Na Mwandishi Wetu**

BIA ya Serengeti Lager imezindua kampeni mpya na ya aina yake itakayowawezesha mashabiki wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kukutana na wachezaji nyota wanaowapenda nje ya uwanja na kufahamu maisha yao nje ya soka.

Kampeni hiyo inayojulikana kama 'Nje ya Dimba na Stars' ambayo ilizinduliwa jana jijini Dar es Salaam, ikilenga kuwapa nafasi mashabiki wa Taifa Stars kukutana na nyota wanaowapenda katika baa zao na pia kutoa fursa kwao ya kuwauliza maswali kuhusu maisha yao nje ya soka pamoja kupiga nao picha za ukumbusho, itakuwa ni kwa nchi nzima huku ikidumu kwa miezi mitatu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, Meneja Mwandamizi wa Chapa ya Serengeti Breweries Limited (SBL), Wankyo Marando, alisema Bia ya Serengeti Lager ikiwa kama shabiki mkuu wa Taifa Stars inajivunia kuwaletea mashabiki wa timu hiyo, nyota inaowapenda na kuwapa nafasi ya kuzungumza



Meneja Mwandamizi wa Chapa ya SBL, Wankyo Marando

nao na hivyo kuwafahamu kwa undani zaidi.

"Shabiki mkuu na mdhamini wa timu yetu ya Taifa, Taifa Stars, Bia ya Serengeti Lager leo inayo furaha kuzindua Kampeni ya Nje ya Dimba na Stars inayolenga kuwakutanisha mashabiki uso-kwa-uso na nyota ambao mara nyingi wamekuwa wakiwaona uwanjani. Hii ni fursa pekee ya mashabiki kujua maisha ya nyota wao nje ya uwanja," alisema Wankyo.

Wankyo alisema kampeni hiyo ya nchi nzima itahusisha wachezaji wa Taifa Stars na kwamba watatembelea mikoa ya Mbeya, Mwanza na Arusha na kukutana na mashabiki wao kupitia matukio kama pati za mwisho wa mwezi 'Nje ya Dimba na Stars' na kwamba kwenye matukio kama hayo mashabiki wataweza kujishindia zawadi mbalimbali na ofa za bei yao pendwa ya Serengeti Lager.

"Wachezaji watakuwa kwenye baa mbalimbali na wakati wateja wetu wa bia ya Serengeti Lager wakiendelea kuburudika na bia yao pendwa iliyotengenezwa kwa kimea kwa asilimia 100 na isiyoongezwa sukari, watapata nafasi ya kuwauliza maswali, kupiga picha na kupata sahihi zao," alisema.

Wankyo aliwataka mashabiki wa Stars kutembelea kurasa za mitandao ya kijamii ya bia ya Serengeti Lager pamoja na kusikiliza redio kwa ajili ya kujua lini na wapi nyota wa Taifa Stars watakuwa.



Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Apansia Lema, akimvisha medali mmoja wa wanariadha wakati wa uzinduzi wa NBC Dodoma Marathon 2021, uliofanyika jana katika Hoteli ya Serena, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# NBC Marathon kukusanya mil.100/- matibabu saratani

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya Sh. milioni 100 zinatarajiwa kupatikana katika mbio za NBC Dodoma Marathon zitakazofanyika Novemba 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, imeelezwa.

Mwakilishi wa Benki ya NBC, William Kallage, ndiye aliyetoa kauli hiyo jana wakati wa uzinduzi wa mbio hizo jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa mwaka huu wameongeza zawadi za washindi, ambapo mshindi wa kwanza wa kilometa 42 kwa wanaume na wanawake kila mmoja ataondoka na Sh. milioni 5.5.

Kallage alisema kwa upande wa kilometa 21, mshindi wa kwanza ataondoka na kitita cha Sh. milioni 3.5, wakati katika kilometa 10, mshindi wa kwanza akikunja kibindoni Sh. milioni 1.5 na yule wa kilometa tano akilamba shilingi milioni moja. Alisema lengo kuu la mbio hizo ni kuchangia huduma za afya katika Hospitali ya Ocean Road, hasa matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi, ambayo yamekuwa yakiua hapa nchini.

Alisema mwaka jana katika mbio hizo zilizofanyika kwa mara ya kwanza, NBC ilichangia Sh. milioni 100 kwa tatizo hilo, na mwaka huu wanataka kuchangia fedha zaidi ili kuhakikisha kinamama wengi wanapata matibabu.

Mwakilishi huyo alisema mbali na viingilio vya washiriki, pia wamekuwa wakipata fedha kutoka kwa wafadhili na wateja wao, ambao nao wamekuwa wakichangia.

Alisema mwaka huu wanatarajia kushirikisha zaidi ya wanariadha 3,000 kutoka mikoa yote ya Tanzania wakati mwaka jana walioshiriki walikuwa 1,944.

Daktari wa Hospitali ya Ocean Road, Crisprin Kahesa, alisema saratani ya mlango wa kizazi ndio ugonjwa unaoua zaidi kwa upande wa saratani, hivyo aliomba watu kusaidia kuchangia matibabu hayo.

Kaimu Katibu Mkuu wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Jackson Ndaweka alisema mwaka huu wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaondoa kasoro zote zilizojitokeza katika mbio za mwaka jana.

Alisema kwa mbio za mwaka huu, zitahusisha pia wanariadha wakubwa kutoka nchi za Kenya, Uganda, Ethiopia pamoja na wa Tanzania ambao wameahidi kushindana.

# Namungo yaiongezea Azam kasi kwa Pyramids

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi wa kwanza kwenye Ligi Kuu Bara msimu huu, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema mechi hiyo imewasaidia kufanyia kazi kasoro zao kuelekea mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Pyramids FC ya Misri.

Azam FC juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo FC kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, hivyo sasa kufikisha pointi nne baada ya kupoteza mchezo mmoja, sare moja na kushinda mechi moja.

Akizungumza na gazeti jijini Dar es Salaam jana, Bahati alisema mchezo wao dhidi ya Namungo, ulikuwa mgumu na wamepambana kupata matokeo mazuri yatakayowasaidia kwa ajili ya mechi ijayo dhidi ya Pyramids.

Alisema wamejipanga vizuri kwa ajili ya kwenda kutafuta matokeo chanya na wanatambua itakuwa mechi ngumu na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu inahitaji kupata matokeo mazuri katika mchezo huo ili kusonga mbele.

"Mechi yetu dhidi ya Namungo FC, imetusaidia kusahihisha mapungufu yetu, kwa sababu tulifanya mabadiliko ya kikosi kwa kuwapumzisha baadhi ya wachezaji, akiwamo Abdallah Kheri (Sebo), ambaye ametumika sana.

"Tunaimani mchezo huu wa ligi umetusaidia kwa sababu Namungo FC wamekuwa washindani wetu wakubwa na mechi hiyo imetusaidia kujiimarisha kwa ajili ya mchezo wa marudiano dhidi ya Pyramids," alisema Bahati.

Alisema hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao, Pyramids huku wakitambua watakuwa na wakati mgumu wa kwenda kutafuta matokeo ugenini.

Azam FC imeondoka jana, usiku kuelekea nchini Misri tayari kukabiliana na wageni wao Pyramids katika mchezo wa marudiano wa CAF, utakaopigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa The 30 June, nchini humo, ikiwa ni baada ya timu hizo kutoka sare tasa katika mchezo wa awali uliopigwa Dimba la Azam Complex, Chamazi.

Ushindi wowote ama sare yoyote ya mabao, yataipa tiketi Azam FC kusonga mbele kusubiri timu moja itakayopangiwa nayo kutoka zile zitakazotolewa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa ili kucheza mechi ya mtoano nyumbani na ugenini na mshindi wa jumla kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## ZISIKUPITE

### MOUNT KULIPWA ZAIDI

CHELSEA wako tayari kumfanya kiungo wake wa England, Mason Mount kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa zaidi wakati klabu hiyo ikijiandaa kuanza mazungumzo ya mkataba mpya na nyota huyo mwenye miaka 22. **(Goal)**

### FATI KUSAINI MKATABA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 18, anakaribia kusaini mkataba mpya wa muda mrefu kusalia klabuni hapo huku kukiwa na kipengele cha ada ya pauni milioni 846 endapo akitaka kuondoka kama ilivyo kwa nyota mwenzake wa Hispania Pedri mwenye miaka 18. **(Fabrizio Romano via Twitter)**

### TRIPPIER KURUDI EPL

BEKI wa kulia wa Atletico Madrid na England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 31, ambaye alikuwa akihusishwa sana na mipango ya kuhamia Manchester United katika majira ya joto, amesema angelipenda kucheza Ligi Kuu England kwa mara nyingine. **(Mirror)**

### SOLSKJAER KUONDOA WATANO

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer ana mpango wa kuondoa angalau wachezaji watano wakati dirisha la Januari likifunguliwa. **(Sun)**

### ADEYEMI NI EURO MILIONI 40

KLABU za Liverpool, Borussia Dortmund au RB Leipzig zitapaswa kulipa kati ya euro milioni 30 hadi 40 kupata saini ya mshambuliaji wa RB Salzburg na Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 19**. (ORF)**

### BRUCE BADO NEWCASTLE

WAMILIKI wapya wa Newcastle United bado hawajazungumza na kocha Steve Bruce baada ya timu hiyo kuchapwa na Tottenham Hotspurs, Jumapili. **(Daily Star)**

### DE LIGT HANA FURAHA JUVE

MLINZI wa Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22, hana furaha pale Juventus, hali inayomsukuma wakala wake, Mino Raiola kufanya mazungumzo na Barcelona kuhusu uwezekano wa kuhamia huko. **(Sport)**

### PEPI KUONDOKA DALLAS

MSHAMBULIAJI wa FC Dallas na Marekani, Ricardo Pepi ameziweka masikio juu klabu kubwa za Ulaya, zikiwamo Liverpool na Bayern Munich kwa kuomba kuondoka rasmi, lakini kinda huyo mwenye miaka 18, ameshakubaliana malipo binafsi ikiwamo mshahara na klabu ya Wolfsburg. **(CBS Sport)**

### ALVAREZ AGOMBEWA ULAYA

ASTON Villa itapaswa kuharakisha kumsajili nyota wa River Plate, Julian Alvarez kwa sababu klabu ya Ligi Kuu Italia, Serie A, AC Milan inamtaka pia mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 21. **(Calciomercato)**

### ROTHWELL ASAINI RANGERS

KLABU za Newcastle United na Leeds United zitamkosa kiungo wa Blackburn Rovers, Joe Rothwell baada ya nyota huyo mwenye miaka 26 kuamua kusaini klabu ya Rangers. **(TEAMtalk)**

### NETO ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham United wanamfuatilia golikipa wa Barcelona, Neto mwenye umri wa miaka 32, ambaye atakuwa tayari kusaini mkataba wa mkopo na kuondoka Nou Camp Januari iwapo klabu itakayomsajili itakubali kumsajili Mbrazil huyo moja kwa moja katika dirisha kubwa la usajili la majira ya joto. **(Sport)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH AWEKA REKODI MPYA LIVERPOOL UEFA

●●● Amefunga katika kila mechi kati ya sita za ugenini kwa Liverpool na ni Aguero pekee ambaye...

**MADRID, Hispania**

MOHAMED Salah amekuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya Liverpool kufunga kwenye mechi tisa mfululizo, wakati akiisaidia timu yake kupata ushindi dhidi ya Atletico Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Liverpool ikiwa nyumbani kwa Atletico waliibuka na ushindi wa mabao 3-2 katika mchezo huo uliokuwa na vuta nikuvute nyingi.

Raia huyo wa Misri aliudokoa mpira eneo la hatari na kuzama wavuni na awali ilionekana kama bao hilo lilifungwa na James Milner.

Hata hivyo, baadaye bao hilo alipewa Salah mwenye umri wa miaka 29 na kumfanya aweke rekodi ya aina yake katika kuzifumania nyavu mfululizo.

Msimu huu Salah alianza kwa kushinda penalti wakati akiwasaidia 'Wekundu' hao kutoka sare ya bao 1-1 na Chelsea, Agosti 28, mwaka huu na kisha kufuata mabao dhidi ya Leeds United, Milan, Crystal Palace, Brentford, Porto (mbili), Manchester City na Watford.

Bao lake dhidi ya Watford Jumamosi iliyopita lilimfanya Salah kuwa mchezaji wa nne wa Liverpool kufunga katika mechi nane mfululizo baada ya Sam Raybould (1902-03), John Aldridge (1987-88) na Daniel Sturridge (2013-14).

Na akawa mchezaji wa kwanza kwenye orodha hiyo baada ya bao lake la Jumanne pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano, huku bao hilo likimfanya kufunga katika kila mechi kati ya sita za ugenini kwa Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ni Sergio Aguero pekee ndiye amefunga kwenye mechi nyingi zaidi za ugenini katika mashindano hayo kwa klabu za Uingereza, ambapo nyota huyo wa sasa wa Barcelona akifunga mara saba wakati akiichezea Manchester City kati ya mwaka 2017 na 2019.

MECHI KALI

HOME AWAY

LAZIO
1.82 | 3.81 | 4.01
MARSEILLE

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 595

# ANCELOTTI AMPIGIA SALUTI VINICIUS



**KIEV, Ukraine**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema Vinicius Junior ameongeza kujiamini baada ya kufunga bao wakati wakiifumua Shakhtar Donetsk, Jumanne.

Mabingwa hao mara 13 wa Ulaya walipata ushindi wa mabao 5-0 mjini Kiev, ukiwa ni mkubwa zaidi ugenini kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu walipoifunga Viktoria Plzen kwa idadi kama hiyo, Novemba mwaka 2018.

Vinicius alifunga mara mbili, huku bao lake la pili akifunga dakika ya 56.

Ancelotti alimpigia 'saluti' mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, ambaye sasa amefikisha mabao saba katika mashindano yote msimu huu, yakiwa mengi zaidi kwa msimu mmoja kwa 'Los Blancos' hao.

Lakini kocha huyo amesisitiza kwamba kujiamini kwa mchezaji huyo kumeongezeka zaidi na sasa wanajiandaa kwa ajili ya Clasico dhidi ya Barcelona, Jumapili.

"Timu yangu imeonyesha nia na molari nzuri, ambapo tumefanya hivyo kwenye kila mechi zilizopita," alisema Ancelotti baada ya mchezo huo.

"Baada ya matokeo ya hivi karibuni, timu iliondekana ikifanya vizuri na tulifanya kile tulichokiahidi.

"Vinicius kwa sasa yupo kwenye kiwango bora zaidi, lakini timu yote ilionyesha kiwango cha hali ya juu kabisa."

# Neville atema nyongo United



**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United ni moja ya timu zisizo na mpangilio kabisa uwanjani, kwa mujibu wa beki wa zamani wa klabu hiyo, Garry Neville.

Zaidi ya hilo, staili wanayocheza Man United na kikosi kinachopangwa kwenda kutekeleza majukumu havina uwiano kabisa.

Neville ametoa maoni yake hayo wakati akizungumzia kiwango cha Man United cha sasa hasa baada ya kufungwa na Leicester City mabao 4-2, wikiendi iliyopita.

Alisema kwamba, yeye asingekubali kuwa beki wa timu yenye Jadon Sancho, Cristiano Ronaldo, Paul Pogba, Bruno Fernandez na Greenwood ndani kwa pamoja, kwani wakiwa na mpira, wakikosa, wakilinda na wakishambulia wanakuwa ovyo kabisa.

"Nilishasema Manchester United itakapoanza kucheza dhidi ya timu 10 za juu, itateseka sana, kwani imekuwa kwenye wakati huo kila inapokutana na timu zilizopangika vizuri," aliandika Neville kupitia ukurasa wake wa Twitter.

Lakini Neville amewamwagia lawama wachezaji wakubwa wa Man United kwamba hawajitumi.

"Ukiwa mchezaji wa daraja la juu, inabidi uonyeshe kuwa wewe ni wa daraja la juu. Jitume hata timu inapopotea hakikisha unaonyesha tofauti," alisema Neville.

5,659,980

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/10/2021 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.33 | 3.41 | 3.01 |
| 02. 23/10/2021 | 17:00 | Millwall vs Stoke City | 2.37 | 3.16 | 2.97 |
| 03. 23/10/2021 | 17:00 | Peterborough vs QPR | 2.90 | 3.20 | 2.39 |
| 04. 23/10/2021 | 17:15 | Cadiz CF vs Alaves | 2.51 | 3.02 | 3.07 |
| 05. 23/10/2021 | 19:30 | Elche vs Espanyol | 2.71 | 3.02 | 2.82 |
| 06. 23/10/2021 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Villarreal | 2.53 | 3.14 | 2.93 |
| 07. 24/10/2021 | 14:00 | Nice vs Lyon | 2.63 | 3.47 | 2.53 |
| 08. 24/10/2021 | 16:00 | West Ham vs Tottenham | 2.38 | 3.36 | 2.96 |
| 09. 24/10/2021 | 16:00 | Brentford vs Leicester | 2.62 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 24/10/2021 | 17:15 | Barcelona vs Real Madrid | 2.65 | 3.54 | 2.53 |
| 11. 24/10/2021 | 18:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.36 | 3.44 | 2.84 |
| 12. 24/10/2021 | 18:30 | Manchester Utd vs Liverpool | 3.07 | 3.62 | 2.21 |
| 13. 24/10/2021 | 19:00 | Roma vs Napoli | 2.62 | 3.43 | 2.62 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 21 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4543 | KRL FC vs Sui Southern Gas Company | 2.07 | 2.85 | 3.82 |
| 14:15 | 4315 | Persik Kediri vs Persipura Jayapura | 2.61 | 3.34 | 2.42 |
| 17:15 | 2682 | Ittihad Kalba vs AL Urooba | 1.68 | 3.96 | 4.05 |
| 17:30 | 2565 | HJK Helsinki vs Maccabi Tel Aviv | 2.89 | 3.29 | 2.44 |
| 17:30 | 4133 | FK Napredak vs Novi Pazar | 1.54 | 3.96 | 5.22 |
| 17:55 | 1213 | AL Baten vs AL Faiha | 3.62 | 3.72 | 1.90 |
| 18:00 | 1300 | Ramtha Club vs Shabab Al Ordun | 1.44 | 4.16 | 6.19 |
| 18:00 | 4344 | AL Aqaba vs Jazeera Amman | 2.23 | 3.20 | 3.00 |
| 18:30 | 3807 | Pro Vercelli vs Giana Erminio | 1.74 | 3.52 | 4.76 |
| 19:30 | 1824 | Al Wasl Dubai vs Al Ain | 2.90 | 3.58 | 2.12 |
| 19:30 | 4646 | AL Wakrah vs Lekhwiya SC | 7.52 | 5.01 | 1.31 |
| 19:30 | 5847 | Petrolul Ploiesti vs CSA Steaua Bucuresti | 2.10 | 3.19 | 3.29 |
| 19:45 | 1136 | Almeria vs Real Sociedad B | 1.52 | 4.04 | 5.92 |
| 19:45 | 1146 | Lazio vs Marseille | 1.82 | 3.81 | 4.01 |
| 19:45 | 1683 | Feyenoord vs Union Berlin | 2.20 | 3.55 | 3.10 |
| 19:45 | 1762 | Ludogorets Razgrad vs Sporting Braga | 3.30 | 3.50 | 2.12 |
| 19:45 | 2540 | Fenerbahce vs Royal Antwerp | 1.73 | 3.85 | 4.50 |
| 19:45 | 2900 | Alashkert Martuni vs LASK Linz | 4.88 | 3.99 | 1.65 |
| 19:45 | 3076 | Midtjylland vs Red Star Belgrade | 2.40 | 3.44 | 2.84 |
| 19:45 | 4043 | Karabakh vs Kairat Almaty | 1.65 | 3.84 | 5.19 |
| 19:45 | 4291 | Bodo Glimt vs Roma | 4.21 | 4.01 | 1.74 |
| 19:45 | 4525 | Vitesse Arnhem vs Tottenham | 4.29 | 4.09 | 1.72 |
| 19:45 | 4562 | NK Mura vs Rennes | 7.59 | 4.80 | 1.39 |
| 19:45 | 4812 | Maccabi Haifa vs Slavia Prague | 3.25 | 3.45 | 2.16 |
| 19:45 | 4843 | Rapid Vienna vs Dinamo Zagreb | 2.62 | 3.57 | 2.51 |
| 19:45 | 5020 | Anorthosis Famagusta vs Flora Tallinn | 1.74 | 3.95 | 4.30 |
| 19:45 | 5284 | Betis vs Bayer Leverkusen | 2.43 | 3.67 | 2.66 |
| 19:45 | 5805 | Copenhagen vs PAOK | 2.14 | 3.47 | 3.29 |
| 20:00 | 1040 | Gais vs AFC Eskilstuna | 2.55 | 3.15 | 2.85 |
| 20:00 | 2425 | AL Tai vs Al Ahli Jeddah | 2.31 | 3.71 | 2.72 |
| 20:00 | 3802 | Zaragoza vs Ponferradina | 2.02 | 3.10 | 3.89 |
| 20:30 | 1915 | Sahab Club vs Wihdat Amman | 8.52 | 4.36 | 1.34 |
| 22:00 | 1343 | Baumit Jablonec vs Randers | 2.59 | 3.24 | 2.74 |
| 22:00 | 1406 | Napoli vs Legia Warszawa | 1.16 | 7.40 | 16.00 |
| 22:00 | 1526 | Lokomotiv Moscow vs Galatasaray | 2.60 | 3.29 | 2.69 |
| 22:00 | 1567 | Sturm Graz vs Real Sociedad | 5.22 | 4.21 | 1.58 |
| 22:00 | 1601 | Slovan Bratislava vs Lincoln FC | 1.25 | 5.54 | 12.24 |
| 22:00 | 1732 | Real Oviedo vs Burgos | 2.09 | 2.92 | 3.95 |
| 22:00 | 1847 | Sparta Prague vs Lyon | 3.40 | 3.70 | 2.02 |
| 22:00 | 2157 | CSKA Sofia vs Zorya Lugansk | 2.29 | 3.21 | 3.21 |
| 22:00 | 2472 | Partizan vs KAA Gent | 2.21 | 3.40 | 3.20 |
| 22:00 | 2697 | Eintracht Frankfurt vs Olympiakos | 1.87 | 3.74 | 3.89 |
| 22:00 | 4417 | FC Basel vs Omonia Nicosia | 1.46 | 4.72 | 6.22 |
| 22:00 | 4851 | Rangers vs Brondby | 1.51 | 4.31 | 6.01 |
| 22:00 | 5139 | Mirandes vs Girona | 2.56 | 3.00 | 2.85 |
| 22:00 | 5198 | Calcio Lecco vs Renate | 2.30 | 3.15 | 3.25 |
| 22:00 | 5258 | CFR Cluj vs AZ Alkmaar | 3.41 | 3.41 | 2.11 |
| 22:00 | 5511 | West Ham vs Racing Genk | 1.34 | 5.18 | 8.16 |
| 22:00 | 5642 | PSV Eindhoven vs Monaco | 2.22 | 3.55 | 3.05 |
| 22:30 | 4048 | Wydad Casablanca vs Olympique Safi | 1.39 | 4.45 | 6.58 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MBAPPE: RAHISI SANA KUCHEZA NA MESSI



**PARIS, Ufaransa**

KUCHEZA na Lionel Messi ni "rahisi" kwa Kylian Mbappe, ambaye anajua kwamba, Paris Saint-Germain lazima iwe kwenye kiwango cha juu zaidi ya kile walichokionyesha dhidi ya RB Leipzig, Jumanne.

Messi alifunga mara mbili na kumfanya kufikisha mabao 123 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati PSG ikitoka nyuma na kupata ushindi wa mabao 3-2 pale kwenye dimba la Parc des Princes.

Wakati akiwa bado hajafunga kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Messi sasa amefikisha mabao matatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu katika klabu yake hiyo mpya, akiwa na idadi sawa ya mabao na Mauro Icardi na Neymar.

Huku Neymar ambaye ni majeruhi akiwa anautazama mchezo huo jukwaani, Mbappe alikuwa na mchango mzuri kwa mabao yote ya Messi mwenye umri wa miaka 34.

Mbappe alianza kuiweka mbele PSG, kabla ya Nordi Mukiele kuwafanya Leipzig kutangulia kwa 2-1 na Messi akasawazisha na baadaye akafunga la tatu kwa mkwaju wa penalti.

Mbappe alikosa penalti katika dakika ya mwisho kabisa ya mchezo huo.

"Tulionana vizuri usiku huu (juzi), ulikuwa wakati mzuri sana," alisema Mbappe akiiambia RMC Sport wakati alipoulizwa kuhusu Messi.

"Sasa Neymar atarudi. Tutatakiwa kuwa vizuri zaidi pamoja, sisi wote watatu. Tutatakiwa kuwa na kiwango bora zaidi, lakini rahisi sana kucheza na Messi."

# Guardiola asifia kiwango Man City



**BRUSSLES, Ubelgiji**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesifia kikosi chake kwa ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Club Brugge kama "moja ya kiwango bora zaidi" walichokionyesha kwenye michuano ya Ulaya.

Riyad Mahrez alifunga mara mbili, huku Joao Cancelo, Kyle Walker na Cole Palmer wakiwa pia kwenye orodha ya wafungaji, wakati Hans Vanaken akiwafungia wenyeji hao.

Kilikuwa ni kiwango bora zaidi walichokionyesha baada ya kupoteza kwenye fainali ya michuano hiyo msimu uliopita na Guardiola anaamini wangeweza kushinda mabao zaidi. "(Ilikuwa) moja ya kiwango bora zaidi katika mashindano ya Ulaya, kwa uhakika kabisa," alisema Guardiola baada ya mchezo huo.

"Niliwaangalia Brugge wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa. Niliangalia mechi zao nyingi, najua namna gani walifanya vizuri dhidi ya PSG.


"Tulipata pasi nyingi kupitia kwa Phil (Foden), tungeweza kufunga mabao mengi zaidi, tulikuwa na nafasi nyingi zaidi. Wote tulifurahishwa na kiwango tulichokionyesha."

Palmer alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa kwa klabu hiyo, na kuwa mchezaji wa kwanza mwenye umri mdogo zaidi kufanya hivyo kwa City, baada ya Foden na Kelechi Iheanacho.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 21, 2021

Nipashe

Salah aweka historia mpya Liverpool Uefa

UKURASA 21

UMETISHA...



Straika wa Twiga Stars, Stumani Ally, akipongezwa na Aisha Masaka kwa kunyanyuliwa juu baada ya kuifungia timu yake bao wakati wakiangukia pua ya mabao 2-1 dhidi ya Namibia kwenye mechi ya kuwania kufuzu Afcon kwa wanawake iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. Aliyeshika mpira akikimbiza kuanza katikati bila kupoteza muda ni Olipa Clement. **MPIGAPICHA WETU**

# NABI ATETEA KUKATA PUMZI KIKOSI YANGA

## ●●●Ni katika mechi dhidi ya KMC FC huku Shikalo naye akitoa sababu kipigo, asema...

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC FC Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema wachezaji wake hawakuishiwa pumzi kipindi cha pili kwenye mechi dhidi ya KMC, bali ilikuwa ni mbinu baada ya kupata mabao mawili ya haraka.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara na kupata ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma, Nabi kupitia kwa Msaidizi wake, Cedric Kaze raia wa Burundi, alisema hakukuwa na ulazima wowote wa kuendelea kukimbizana kwani tayari walikuwa wameshapata mabao mawili, hivyo kazi iliyobaki ilikuwa ni kuyalinda tu.

"Tumeshafunga mabao mawili dakika 15 za mwanzo, ilikuwa ni lazima tutulie, kwanza tupo ugenini, tuliocheza nao ndiyo walitakiwa kuwa na presha na sio sisi, si kweli kusema eti pumzi imepungua, hata ukifanya tathmini, sisi ndiyo tuliomiliki zaidi," alisema.

Wachambuzi na wataalamu wa masuala ya soka, wanadai kuwa wachezaji wa Yanga huanza kwa kwa kasi, lakini huanza kupungua taratibu kadri muda unavyozidi kwenda na hii yote inaonekana kuwa wanaishiwa pumzi, hasa kuanzia dakika ya 60.

Msimu huu, Yanga haijawahi kufunga bao kipindi cha pili, ingawa pia haijaruhusu bao lolote kuanzia mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba, hadi mechi tatu za Ligi Kuu.

Kaimu Kocha wa KMC, Hamad Ally, alisema wamepoteza mechi hiyo kutokana na umakini hasa kipindi cha kwanza.

"Tulifanya makosa kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili tulibadilika na kupata nafasi ambazo hatukuzitumia na hilo tutakwenda kulifanyia kazi.

Wakati huo huko, kipa wa KMC, Farouk Shikalo, amesema walifungwa na Yanga, baada ya kuzidiwa eneo la katikati hasa kipindi cha kwanza.

"Walimiliki katikati, unajua Yanga ni timu kubwa na ina wachezaji wazoefu, wakatuwahi, mimi peke yangu nisingeweza kuzuia, walipata nafasi zile wakatufunga, baadaye tulipojirekebisha walikuwa tayari wanaongoza kwa mabao mawili," alisema kipa huyo ambaye msimu uliopita alichezea Yanga.

Yalikuwa ni mabao ya Fiston Mayele likiwa ni la kwanza kwake kwenye Ligi Kuu msimu huu na Feisal Salum ambaye ni bao lake la pili, moja akilifunga kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba.

Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi tisa baada ya michezo mitatu, itashuka tena dimbani Oktoba 30, mwaka huu kuikaribisha Azam FC katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Azam jana usiku ilikwea pipa kuelekea Misri tayari kwa mechi yao ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Pyramids baada ya wiki iliyopita timu hizo kutoka sare tasa katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

## Straika wa Sevilla aiua Twiga Stars

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na straika anayecheza soka la kulipwa timu ya wanawake ya Sevilla ya Hispania, Zenatha Coleman, jana yaliiua Twiga Stars baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Namibia katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Straika huyo hatari alifunga bao moja kila kipindi kwenye mechi ya kutafuta tiketi ya kufuzu kucheza fainali za mataifa ya Afrika (Afcon) kwa wanawake zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Ilikuwa ni pasi ndefu iliyopigwa katikati ya uwanja, ikawapita mabeki w wawili wa Tanzania, kabla mfungaji hajachomoka na kubetua mpira kwa ufundi baada ya kipa Jeneth Shija kutoka golini akijaribu kuuwahi, lakini aliishia kushuhudia bao hilo la kwanza likizama kimyani dakika ya 21.

Twiga Stars ilibidi kusubiri hadi dakika ya 40 kusawazisha bao hilo, shukrani kwa mkwaju wa mbali wa kushtukiza ulioachiwa na Stumani Ally na kutinga moja kwa moja nyavuni.

Stumai aliachia mkwaju huo juu akiwa takribani umbali wa mita 35, baada ya kupiga mpira wa juu ulioshukia golini na kutumbukia nyavuni.

Lakini alikuwa ni Zenatha tena dakika ya 60, alipofunga bao la pili kwa faulo ya mbali ambayo aliipiga kiufundi na kujaa wavuni, huku kipa Shija akidhani unatoka, lakini hata alipochupa kutaka kuokoa, haikuwezekana tena kuwahi kasi ya mpira, hivyo kujaa nyavuni na kuifanya Namibia kuwa mbele kwa mabao mawili.

Hata hivyo, kama Aisha Masaka angekuwa makini angeweza kuisawazishia Twiga Stars bao baki ya 77, baada ya kupiga kichwa juu mpira wa kona uliopigwa na Enekia Kasonga, huku dakika moja kabla ya mechi kumalizika, Kisisa naye akipiga mpira wa juu uliokuwa unamiminika wavuni lakini kipa Melisa Methius aliupangua.

Twiga sasa italazimika kwenda kushinda ugenini Jumamosi ili kusonga mbele.

Timu itakayopata matokeo ya jumla itakutana na mshindi wa jumla kati ya Malawi na Zambia na mshindi wa mchezo huo ndiye atakayefuzu fainali hizo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >